**4 JUNI, 2026**

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA TATU

**Kikao cha Arobaini na Tatu — Tarehe 4 Juni, 2026**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

**MASWALI KWA WAZIRI MKUU**

**SPIKA:** Maswali kwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, karibu.

Mheshimiwa Haran Nyakisa Sanga, Mbunge wa Kigamboni.

**MHE. HARAN N. SANGA:** Mheshimiwa Spika, kwanza ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali kwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Waziri Mkuu kwanza ninakupongeza sana kwa kazi nzuri ambayo unafanya katika kutatua changamoto mbalimbali za wananchi hapa Tanzania. Hata mimi nilivyokuwa nina shida zangu za kivuko pale Kigamboni nikakwambia ukaniambia kesho nakuja, na ulifika ukaongea na wale

wananchi. Ninakupongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na wimbi kubwa la kukua kwa miji mikuu kama Arusha, Mwanza, Mbeya, Dodoma na Dar es Salaam; inakua kwa kasi kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, ninataka nijue, nini kauli ya Serikali katika kuimarisha miundombinu hususani ya kiwango cha reli ili kufanya miji hii iweze kukua kwa kasi kuendana na idadi ya wananchi, lakini pia kuongeza uchumi/kuchachua uchumi katika majiji haya hususan Jiji la Dar es Salaam? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa nafasi hii ili niweze kujibu swali zuri la Mheshimiwa Haran Sanga, Mbunge wa Kigamboni, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kabla sijajibu swali lake ninaomba uniruhusu niseme mambo mawili; jambo la kwanza ninaomba nitumie Bunge lako Tukufu kuwapongeza vijana wetu wa *Serengeti Boys* kwa hatua kubwa na yenye heshima waliyofikia katika mashindano ya vijana chini ya miaka 17, kwa kucheza hatua ya fainali tena yenye ushindani na kukosa tu bahati kwa kweli ya kulileta kombe hilo hapa nyumbani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninajua Watanzania watakuwa wamesikitika, lakini ninawatoa hofu, kwa sisi wafugaji ukiona kila siku wingu kubwa linakuja na mvua hainyeshi, kuna siku mvua itanyesha hata bila kuwa na wingu kubwa.

Mheshimiwa Spika, Yanga walikosakosa wakatolewa kwa uwiano wa magoli, Simba wakakosakosa kwa kushindwa tu mbinu za nje ya uwanja, na vijana jana wamekosa. Kuna siku kombe hilo linakuja na wala siyo siku nyingi litakuja hapa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili, ninatoa rai kwa Bunge lako Tukufu, wiki ijayo tarehe 11 Juni, siku ya Alhamisi itawasilishwa Bajeti Kuu

ya Serikali hapa Bungeni. Ninatoa rai kwa Waheshimiwa Mawaziri na Wabunge wote kushiriki katika siku hiyo ya kusomwa Bajeti Kuu ya Serikali, lakini pia na katika majadiliano ya Bajeti Kuu ya Serikali. Bajeti Kuu ya Serikali ni bajeti ya nchi inayogusa maisha ya kila Mtanzania na mpaka majirani zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maeneo hayo mawili, sasa ninaomba nijibu swali la Mheshimiwa Haran Sanga kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ninampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kuleta swali hilo. Ni kweli kuna kasi kubwa ya kukua kwa miji yetu kama alivyoitaja na kusababisha msongamano pamoja na kupoozesha shughuli za kiuchumi na kuongeza gharama za maisha.

Mheshimiwa Spika, pendekezo alilolitoa Mheshimiwa Mbunge ni moja ya hatua zinazostahili kuchukulia ili kuweza kupata ufumbuzi wa tatizo la aina hiyo na kurahisisha shughuli za kiuchumi kama Mheshimiwa Mbunge alivyosema.

Mheshimiwa Spika, tayari Serikali imeanza kuchukua hatua; moja ikiwa ni kuchukua hatua za sasa za kuondoa misongamano katika miji yetu inayokua, na hatua hizo ambazo zimeanza kuchukuliwa kwa sasa ni kuongeza idadi ya barabara za ndani na kuzijenga kwa kiwango cha lami barabara za mitaa.

Mheshimiwa Spika, hatua nyingine inayochukuliwa imekuwa ya kujenga njia za mzunguko ili magari ambayo hayana ulazima kupita katikati ya miji hiyo yasipite, bali yatumie njia za mzunguko. Tumeshafanya hivyo kwa hapa Dodoma, ujenzi unaendelea kwa Iringa, ujenzi ulishakamilika kwa Arusha. Tuna mpango huo na shughuli zinaendelea kwa Mwanza, tuna mpango kama huo na shughuli zainaendelea kwa Mbeya; tuna shughuli ya aina hiyo Mkoa wa Ruvuma na maeneo mengine mengi ambako *bypass* zinajengwa. Kusudi lake ni ku-*decongest*, kuondoa misongamano katikati ya majiji yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hatua itakayofuata ni hiyo ya kuwa na reli kwenye majiji yetu na hatua za awali zimeshaanza. Katika baadhi ya mikoa kuna hatua za upembuzi zinaendelea, katika baadhi ya mikoa maandiko yanafanyika, lakini pia wakati hatua hizo zinaendelea Serikali inajipa muda wa kukamilisha miradi mikubwa ya kimkakati ya reli ambayo na yenyewe kusudi lake kubwa ni hilo hilo la kuweza kufungua uchumi, kama ambavyo mnajua Dar es Salaam – Dodoma *operations* zimeshaanza, lakini bado tunakazi ya kufungua hivi vipande viwili mpaka Tabora, Dodoma – Tabora; lakini pia na vipande viwili, kimoja cha katikati cha Tabora – Isaka, Isaka – Mwanza tuko hatua nzuri tunaelekea 70% sasa, lakini pia cha Tabora – Kigoma, Kigoma kuelekea nchi za jirani ya Burundi, lakini pia tuna kipande kingine cha kutokea Kaliua kwenda mpaka kule Mpanda.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kadiri hatua za kifedha zinavyoruhusu tutarejea kuwekeza pia kwenye ujenzi wa zile reli za ndani ya majiji yetu ili kuweza kufungua uchumi ndani ya majiji yetu. Serikali iko wazi kutumia hata njia za ubia katika kujenga reli hizo, sambamba na zile za mikoa mingine ambazo zimebainishwa katika ilani ya uchaguzi.

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Kaiza.

**MHE. AGNESTA L. KAIZA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ili nami siku ya leo niweze kumuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu swali.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa Mheshimiwa Waziri Mkuu ninaomba pia nitumie nafasi hii kukupongeza sana kwa kazi nzuri unayoifanya ya kumsaidia Mheshimiwa Rais kwa ajili ya kuwafikia wananchi na kutatua kero zao. Ninakumbuka ulikuja Mkoa wa Dar es Salaam kwa udharura, lakini hakika uliacha tabasamu na bado tunakusubiri kwa hamu uje jimbo kwa jimbo, ili wananchi waweze kupata tabasamu moja kwa moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa, swali langu ni kama ifuatavyo: Mheshimiwa Waziri Mkuu, nchi yetu imekuwa ikifanya chaguzi za halmashauri katika ngazi ya Udiwani kwa namna iliyo tofauti na

nafasi nyingine, kwa maana kwamba nafasi Meya na Mwenyekiti wa Halmashauri hufanyika kila baada ya miaka mitano, lakini nafasi ya Naibu Meya na Makamu Wenyeviti wa Halmashauri hufanyika kila baada ya mwaka mmoja.

Mheshimiwa Spika, uchaguzi huu wa kila mwaka haujawahi kuizacha salama halmashauri zetu pamoja na Madiwani, kwani chaguzi hizi hupelekea misuguano, migongano, na jambo ambalo linapelekea hata utendaji kazi wa Madiwani wetu katika halmashauri kuzorota sana kwa sababu kila baada ya uchaguzi mmoja wao huanza kuingia katika michakato ya kampeni na hivyo shughuli za halmashauri kuzorota. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa kwa nia njema ile ile ya Serikali ambapo Mheshimiwa Waziri Mkuu, mmekuwa mkifanya marekebisho kwenye sheria mbalimbali na kanuni mbalimbali, je, Serikali haioni umuhimu sasa wa kuleta marekebisho kwa hati ya dharura kabisa ili chaguzi hizi za hawa viongozi ziwe zinafanyika kila baada ya miaka mitano ili kuondoa hii sintofahamu ambayo kwa kweli halmashaur zetu Mheshimiwa Waziri Mkuu haziko katika hali nzuri? Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kujibu swali hili la Mheshimiwa Agnesta Lambert Kaiza, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Agnesta ameleta swali zuri na ni ukweli alichosema, ndiyo mambo yanayotokea katika halmashauri nyingi. Nadhani siku za nyuma pengine nafasi hiyo haikuchukuliwa kama nafasi rasmi sana, kwa hiyo, ilichukuliwa tu kwamba kwenye kikao kimojawapo tu kwa urahisi hivi Madiwani watakusanyika tu, watamchukua mmoja wapo awe Makamu Mweyekiti kwa ajili ya kumsaidia Mwenyekiti au Makamu Meya kwa ajili ya kumsaidia Mstahiki Meya.

Mheshimiwa Spika, kiuhalisia ni kweli imekuwa chanzo cha migawanyiko na chanzo cha migogoro katika maeneo mengi.

Sasa inageuza kwamba shughuli inakuwa uchaguzi badala ya shughuli zile ambazo zinafanywa na uongozi huo unaopatikana. Kwa sababu hiyo, pana mantiki ya kuliangalia upya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata Bunge lako Tukufu, Wenyeviti wa Kamati wanachaguliwa Kamati zinadumu, ifikapo nusu ya uhai wa Bunge ninadhani ndiyo kunakuwa na uchaguzi mwingine wa Makamu. Mwenyekiti akishachaguliwa anakaa katika kipindi hiki cha uhai wa Kamati.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeona *logic* hii na nimepita mahali nimesema mara kadhaa, na nimeshamwelekeza Mheshimiwa Waziri wa Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia mambo ya TAMISEMI na bahati nzuri na Mwanasheria Mkuu wa Serikali yupo, wakae na Mwanasheria Mkuu waiangalie upya sheria hiyo ili waweze kuleta mapendekezo kwa haraka, ikiwezekana Bunge lijalo ambalo litakuwa linapitia miswada, ili tuweze kuiangalia upya sheria hiyo na Bunge lako Tukufu liweze kufanya marekebisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa Tanzania katika kuzunguka nimekuja kugundua wana kero nyingi ambazo nyingine zinaweza zikashughulikiwa ngazi za halmashauri, kama kila kamati itatimiza wajibu wake. Haya mambo yote wanayoyatoa pale yana kamati zake. Kamati zetu zingekaa vizuri na zikafuatailia mambo ya aina hiyo na zikapendekeza, kero hizi zingetatuliwa kitaasisi ambao ndiyo msingi wa utawala bora. Kutatua kero kitaasisi badala ya kutatua kwa dharura.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hii ni hoja ya msingi na nadhani panapo uzima tutakamilisha na huenda Bunge linalokuja tukawa na mapendekezo hayo ili Bunge lako Tukufu liweze kupitisha marekebisho haya. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, na sisi kama Wajumbe kwenye halmashauri zetu twendelee kusimamia misingi hii. Kwamba, uchaguzi umepita watu wote wajikite kwenye kufanya kazi. Tusiwe na nchi na wananchi wanaowaza uchaguzi kila siku. Uchaguzi si

kazi, kuna kazi tunazotakiwa kufanya ili wananchi waweze kupata maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninayasema kwa wale Makamu ambao kila wakati wanagombea, lakini wapo pia hata wale Wenyeviti, anaapishwa leo uenyekiti wa halmashauri siku hiyo hiyo anaanza kampeni ya kutafuta Ubunge. Kila mtu afanyie kwanza kazi nafasi aliyopewa na ili watu waione kazi, waione kazi. Waione hiyo kazi na kama wananchi watakuwa wameridhika na hiyo kazi, watasema ndiyo huyu alikuwa Mwenyekiti wa Halmashauri, lakini kwa sasa tunahisi anaweza akawa Mbunge, lakini siyo unaapishwa tu kesho yake unaanza kila siku unatoa rushwa sasa isiyojulikana na inayojulikana ili Madiwani wakuone wewe ndiyo Mbunge wakati Mbunge yupo, au ili Madiwani wakuone wewe ndiyo Makamu Mwenyekiti wakati Makamu Mwenyekiti yupo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii si kitu kizuri kwenye nchi ambayo wananchi wake wanakiu na maendeleo na siyo kiu ya kubadilibadili Mwenyekiti au Makamu Mwenyekiti ama Mbunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa nafasi hii. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Sara Msafiri.

**MHE. SARA M. ALLY:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niulize kwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, na mimi ninachukua nafasi hii kukupongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi kubwa unayoifanya ya kumsaidia Mheshimiwa Rais kutatua kero za wananchi na ninakushukuru sana wananchi wa Jimbo la Mvomero umewakimbilia walivyopata mafuriko, uliwaletea chakula cha kutosha na huduma za dharura.

Mheshimiwa Waziri Mkuu nina swali, kama tunavyojua Dira ya Maendeleo ya Taifa imelenga itakavyofika mwaka 2050 uchumi wetu wa Pato la Taifa ufikie dola trilioni moja.

Mheshimiwa Spika, tunajua kwamba wananchi wengi wako vijijini na wanategemea kilimo katika kuongeza tija na kuongeza ukuaji wa uchumi, lakini tunajua kwamba zipo changamoto nyingi kwenye sekta ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, je, Serikali sasa ina mpango gani kuwekeza kikamilifu kwenye kilimo cha umwagiliaji ili kuongeza uzalishaji na kuweza kuchochea ukuaji na kuongeza viwanda na masoko na kuweza kufikia dhana hiyo ya ukuaji wa uchumi kwa sababu Sekta Binafsi itachangia 70% ya ukuaji wa dira hii? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa nafasi hii ili niweze kujibu swali la Mheshimiwa Sara Msafiri kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Sara Msafiri ameleta swali zuri sana, ninampogeza sana. Kimsingi Kilimo cha Umwagiliaji kwa nchi ambayo zaidi ya 65% na kuendelea ya wananchi wake wakiwa wanajishughulisha na kilimo, ni ufumbuzi wa matatizo mengi. Moja, kilimo cha umwagiliaji kinaleta dhana halisi ya kukua kwa lile pato la mtu mmoja mmoja kiuhalisia badala ya wastani.

Mheshimiwa Spika, tunapopima masuala haya ya pato la mtu tunatumia wastani. Ukisema anapata dola 1,000 kwa siku ama *per capita income* yake ni hii, kwa kiwango kikubwa inakuwa wastani, lakini uwekezaji katika sekta ya umwagiliaji unaenda kukuza kipato kwa uhalisia cha mtu mmoja mmoja. Serikali imeanza kuchukua hatua hizo. Nimesema mojawapo ni hilo la kipato.

Mheshimiwa Spika, la pili, umwagiliaji unaenda kutoa suluhisho, kama mkulima alikuwa akilima mara moja kwa mwaka, anaingia kwenye shida ya uhaba wa chakula anahitaji chakula cha msaada, mkulima huyo jawabu analotakiwa kupewa siyo kupewa chakula tu cha msaada kila wakati, anatakiwa

awezeshwe alime mara mbili ili chakula kiweze kutosheleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, katika nchi yetu kumekuwa na migogoro mingi ya ardhi, migogoro mingi kati ya wakulima na wafugaji, migogoro mingi kati ya vijiji na maeneo yaliyotengwa ya hifadhi na vinginevyo.

Mheshimiwa Spika, hii na yenyewe inatuambia kwamba ongezeko la watu ni kubwa na ardhi haiongezeki. Maana yake lazima iwepo njia ya kutumia, njia ya tofauti ya matumizi ya ardhi, kwamba badala ya kila siku kuongeza mashamba ili uongeze uzalishaji inatakiwa ije njia ya kuongeza uzalishaji kwa kutumia eneo lile lile kwa sababu ardhi haiongezeki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua hilo, Serikali inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, imechukua jitihada za makusudi na za vitendo kwa kuongeza bajeti ya Serikali inayokwenda kwenye kilimo kwa zaidi ya mara tano na baada ya bajeti hiyo kuongezeka, sehemu kubwa imeelekezwa kwenye miradi ya umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, imefufuliwa miradi ya umwagiliaji ambayo ilikuwa imejaa tope na mingineyo ikiwa imevunjika vunjika, maeneo mengi imefufuliwa miradi hiyo ambapo kwa sasa tuna zaidi ya miradi 780 ambayo imefanyiwa kazi na mingine inaendelea kufanyiwa kazi na mingine ipo hatua mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, pia, Serikali imewekeza kwenye uendelezaji wa mabonde, kama mnavyojua nchi yetu huwa imegawanywa katika mabonde ambapo mengi kati ya hayo mabonde yameingia kwenye hatua za uendelezaji.

Mheshimiwa Spika, moja kubwa ambalo ni la muda mrefu na linaendana na dira ambayo Mheshimiwa Sara ameitaja, ni kwamba Serikali katika dira na katika ilani yake hii mpya, imeelekeza kwenye kuwekeza kwenye Gridi ya Maji ya Taifa ambapo tunayatoa maji kwenye vyanzo visivyokauka, mfano wa

Ziwa Victoria, Tanganyika, Nyasa, mito mikubwa, kuipeleka kwenye Gridi ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, maelekezo ya Mheshimiwa Rais na maelekezo ya ilani ni kwamba sasa tunapounganisha maji kutoka kwenye vyanzo hivyo vya kudumu, tusipeleke tu maji hayo kwa ajili ya matumizi ya majumbani, bali kuwe na matoleo kwa ajili ya umwagiliaji, lakini pia na shughuli za ufugaji katika maeneo husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo hili ni jambo ambalo litaenda kutekeleza hili swali na maoni makubwa aliyoyaleta Mheshimiwa Mbunge. Kutakuwa na miradi mikubwa kila ukanda ambapo kuna chanzo cha kudumu cha maji.

Mheshimiwa Spika, tutapeleka kwenye miradi ya maji ya majumbani kwa matumizi ya kila siku, lakini pia kutakuwepo na matoleo ya maji kwa ajili ya umwagiliaji na matumizi ya mifugo kwa ajili ya shughuli hizo zinazoendelea katika maeneo husika ambapo miradi hiyo mikubwa inapita.

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Asha Salum Motto.

**MHE. ASHA S. MOTTO:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi ya kumuuliza swali Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninakupongeza sana kwa kazi kubwa unayoendelea kuifanya ya kutatua changamoto mbalimbali kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, niipongeze sana Serikali kwa kuboresha miundombinu ya afya na uhakika wa dawa na vifaa tiba nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri Mkuu, hivi karibuni kumeibuka na taarifa za kuenea kwa ugonjwa wa ebola kwa baadhi ya nchi za jirani na kwa kuwa nchi yetu inamahusiano mazuri sana na nchi hizi za jirani, kwa maana ya kibiashara na mahusiano ya kijamii.

Mheshimiwa Spika, je, Serikali imejipangaje kudhibiti na kukabiliana na janga hili la ebola? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa nafasi hii na nijibu swali la Mheshimiwa Asha Motto, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa kulileta swali hili kwa wakati, ni jambo ambalo linaendelea katika maeneo mbalimbali hapa Afrika.

Mheshimiwa Spika, kwanza nitumie Bunge lako Tukufu kusema mpaka sasa tupo salama, nchi yetu ipo salama, ni jambo la kumshukuru Mungu, tupo salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge, nchi yetu inamahusiano mema na siyo tu ya Kiserikali, ya watu na watu mipakani na pia Tanzania siyo kisiwa na jambo hili ni jambo la mlipuko inayotokea maeneo mbalimbali. Ni jambo linaloweza kutokea katika nchi yoyote.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kutambua hilo tumeendelea kuchukua hatua za kutoa elimu na nitumie Bunge lako Tukufu, kuendelea kupaza sauti kwa Watanzania wote kuendelea kuchukua tahadhari kama ambavyo tumekuwa tukichukua tahadhari yanapotokea mambo ya magonjwa ya aina hii ambalo hili siyo la kwanza na hata hili hili la aina hii la ebola siyo la kwanza kutokea katika mataifa haya ambayo yameripotiwa kuwa na tatizo hilo.

Mheshimiwa Spika, tuendelee kuchukua hatua za tahadhari, tuendelee kuelimishana, lakini pia tuwe na utayari, mtu anapotoka nje ya nchi, anapotoka nje ya mipaka; awe mtanzania, awe mgeni tuwe na utayari wa kufanya vipimo na tuwe na utayari wa kutokuficha tetesi hizo, lakini pia na kutokuficha dalili hizo ili kuweza kupata huduma ya kwanza ambayo itasaidia kutokuruhusu ugonjwa kusambaa endapo kuna

mgeni ama dalili zozote ama tetesi zitakazojitokeza katika eneo lolote lile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa undani zaidi, Waziri wa Afya, Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa, pamoja na timu yake ya wataalam wanajipanga kuendelea kutoa elimu hii, lakini pia na kutoa taarifa kuhusu hali halisi ya jambo hilo ndani ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mungu ni mwema bado tupo salama, tuendelee kumuomba Mungu, hajawahi kushindwa, tumewahi kuvuka mambo mengi magumu ya aina hii na hata hili tutavuka salama. Tuendelee kuzingatia yale ambayo wataalam wetu wa afya watatushauri, tuyazingatie na tuyafanyie kazi ili kuweza kuepuka madhara yanayoweza kujitokeza. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Dickson Nathan Lutevele.

**MHE. DICKSON N. LUTEVELE:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa kunipa nafasi na mimi ya kuuliza swali kwa Serikali, lakini kabla sijauliza, ninaomba nichukue nafasi hii kumpongeza sana Waziri wetu Mkuu, kwa kazi kubwa anayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri Mkuu, kimsingi ziara unazozifanya siyo tu zinaweka ukaribu kati ya wananchi na Serikali yao, lakini zinaongeza mahaba sana kwa wananchi kwa Serikali yao, hasa pale yanapotatuliwa papo kwa papo matatizo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa ninaomba nimuulize Mheshimiwa Waziri Mkuu, swali; sekta ya kilimo imekuwa na mchango mkubwa sana katika kuongeza pato la wakulima, lakini pia katika kuongeza pato la Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na utaratibu wa malipo baadaye hasa kwenye mazao ya kilimo cha biashara kama chai na hii imepelekea sana wananchi hawa baada ya kupeleka mazao yao viwandani wanacheleweshewa sana malipo na wakati mwingine hawalipwi kabisa. Nimetoa mfano kwenye zao la chai.

Mheshimiwa Spika, sasa nini mpango wa Serikali katika kuhakikisha kwamba wananchi hawa wanakuwa wanalipwa kwa wakati na hivyo kuendeleza mashamba yale ambayo mazao yanatoka na kuongeza pato lao? Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii nijibu swali la Mheshimiwa Mbunge wetu wa Mafinga, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Lutevele, ameleta jambo ambalo linajitokeza siyo tu kwa zao la chai, linajitokeza pia kwa mazao mengine.

Mheshimiwa Spika, nimefanya vikao na wadau wakiwemo Waheshimiwa Wabunge na hata yeye mwenyewe Mheshimiwa Lutevele, pamoja na Wabunge wenzake wanaotokea ukanda wa chai, tumeshakaa vikao takribani viwili/vitatu tukiwa pia na Waziri wa Kilimo pamoja na wataalam wake.

Mheshimiwa Spika, tumekaa pia na Wabunge wanaotokea upande wa zao la tumbaku, tumekaa na Wabunge wanaotokea eneo la zao la pamba na mazao mengine; korosho na mazao mchanganyiko.

Mheshimiwa Spika, kumekuwepo na tatizo hilo na hasa hasa katika miaka ya hivi karibuni kumekuwepo na kupanda na kushuka kwa bei hizi na wakati mwingine ucheleweshaji wa malipo kwa sababu kule sokoni tunapotegemea maeneo mengi kumekuwa kukitokeza na kuharibika kwa mnyororo huu wa ugavi.

Mheshimiwa Spika, utakumbuka hapajatulia huko kwenye masoko yetu kwa mfululizo linatoka hili linaingia lingine. Imekuja UVIKO-19 kukawa na *lockdown;* kukishakuwa na *lockdown* mnyororo wa ugavi unaharibika kule duniani. Baada ya hapo kukatokea mzozo wa Ulaya ya Mashariki, baada ya hapo kukatokea tatizo lile lililokumba uhaba wa fedha za kigeni katika

mataifa mengi na sasa ukatokea tena huu mzozo wa Mashariki ya Mbali/Mashariki ya Kati.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, Serikali imeendelea kujitahidi kuhakikisha kwamba wakulima wanapata masoko, lakini pia wanapata bei zinazostahili katika masoko yake.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya hatua ambazo Serikali imeendelea kuchukua ni kufanya mahusiano ya nchi na nchi zile ambazo tunashirikiana katika ununuzi wa mazao husika ili kuweza kuhakikisha kwamba kampuni zinayotoka katika nchi hizo ambazo zinanunua mazao yale ambayo wakulima wetu wanayalima ikiwemo chai, wanaendelea kupata faida kutokana na kilimo chao.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia inachukua hatua kupitia Wizara ya Viwanda na Biashara, kuhamasisha upatikanaji ama kuanzishwa kwa viwanda vya kuchakata mazao haya ndani ya nchi yetu, kwa sababu mazao yenyewe kama chai yana muda mfupi sana kabla hayajaharibika yasipochakatwa. Hatua hiyo imeshachukuliwa kwa upande wa mazao ya Kaskazini, Mashariki kule Tanga, kuna kiwanda kinafungwa siku siyo nyingi kwa jitihada za Serikali ili kuweza kuhakikisha kwamba unapunguza uharibifu lakini pia unatengeneza uchakatajwi wa zao la chai katika eneo husika.

Mheshimiwa Spika, hivyo hivyo na kwa upande wa Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini, ikiwemo Mafinga hatua zinaendelea kuchukuliwa za kufufua viwanda vile; majadiliano yanaendelea na wawekezaji waliopo na wanunuzi wale ambao wamekuwa wakinunua ili kuweza kuhakikisha tunashughulikia tatizo hilo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge pamoja na Wananchi wake wa Mafinga, Mungu akitupa uhai *weekend* hii tutakuwa kwake Mafinga kule na tutakuwa na timu nzima ya Serikali ikiwemo Wizara inayoshughulikia suala hilo. Tutaendelea kutoa mrejesho kwa wananchi wake ili kuweza kuhakikisha kwamba wananchi hao wanapata faida kutokana na nguvu

kubwa wanayoweka kwenye zao hilo, ambalo ni zao lao la msingi la kuwaletea maendeleo.

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Ali Hassan Omar King.

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kupata nafasi hii ya kuuliza swali kwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, nchi yetu imekuwa inafanya utaratibu na jitihada mbalimbali katika kukaribisha wawekezaji wa kigeni kwa jitihada kubwa ambazo tunaziona kama vile viongozi wetu kutoka nje ya nchi kufanya mialiko, mabalozi wetu kutumia *economic diplomacy,* lakini hata jitihada za ndani *TISEZA* wanazofanya kwa vivutio tofauti, lakini baada ya uwekezaji kunakuja kujitokeza vikwazo vya kikodi, kwa kusema kwamba tunawalinda wawekezaji wa ndani.

Mheshimiwa Spika, je, Serikali ina mkakati gani ambao utafanya kuwawezesha wawekezaji wa ndani bila ya kuweka vikwazo vya kikodi kwa wawekezaji wa nje. Tukiamini kwamba *foreign direct investment* ina asilimia kubwa sana katika dira yetu katika kukuza uchumi wa nchi yetu? Ninashukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa nafasi na nimpongeze Mheshimiwa King, kwa swali zuri.

Mheshimiwa Spika, kumbuka Mheshimiwa King, amekuwa kwenye Kamati ya Bajeti, amekuwa kwenye kamati mbalimbali zinazoshughulikia masuala ya kiuchumi kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, hoja aliyoitoa Mheshimiwa Mbunge ni ya msingi na kimsingi hivi ndivyo ambavyo Serikali imekuwa ikifanya na tutaendelea kurekebisha kama bado kuna dosari zinajitokeza.

Mheshimiwa Spika, tunahitaji uwekezaji wote, uwekezaji wa ndani na uwekezaji wa nje. Maeneo ambapo kunakuwepo na hoja za kikodi, kimsingi hakulengi sana kwamba ni kwa ajili ya

kulinda wawekezaji wa ndani. Maeneo ambayo yanahusisha masuala ya kikodi kumekuwa na vivutio ambavyo wawekezaji wa nje wanapata vingi tu ambavyo wamekuwa wakivipata.

Mheshimiwa Spika, wawekezaji mahiri, wawekezaji mahiri maalumu na wamekuwa wakipewa taratibu za kufuata. Hata hivyo katika siku za hivi karibuni tumeongeza tu maboresho kwamba tusivutie peke yake wawekezaji wa nje, kuna umuhimu wa kuvutia pia wawekezaji wa ndani. Kwa hiyo, na wenyewe tumewawekea utaratibu pamoja na viwango vilevile vya mitaji ambayo zamani ilikuwa inalinganishwa na yule anayetoka nje.

Mheshimiwa Spika, sasa kumekuwa na dirisha mahsusi kwa wawekezaji wa ndani na kumekuwa na viwango maalumu kwa wawekezaji wa ndani ili kuweza kuwafanya wakidhi, tukiwa tumeanza na kiwango cha chini cha dola laki moja, katika sheria ya juzi ile tuliyoitunga ya Uwekezaji na Maeneo Maalum ya Uwekezaji. Sasa tumeshusha iwe dola 50,000 kwa wawekezaji wa ndani.

Mheshimiwa Spika, kitu peke ambacho tulikiweka kisheria kinachohusu Watanzania ilikuwa ni kwenye hizi shughuli za uzalishaji, ujenzi na kwingineko. Tuliona kuna umuhimu wa kujenga sekta binafsi ya ndani. Sheria ya zamani ilikuwa inasema, watanzania wanaweza tu wakachukua asilimia kadhaa kwenye mradi, labda 30 au kupitia *local content* na sheria yenyewe ilikuwa inasema kwamba miradi yote ile lazima ifanywe na wageni.

Mheshimiwa Spika, wageni wengine walikuwa na uwezo sawasawa na Watanzania. Wengine walikuwa hata wanauwezo chini ya Watanzania, lakini walikuwa wanapata sifa tu ya kupewa mradi kwa sababu wao ni wageni. Hii haikuwa imekaa sawa, Mheshimiwa Rais alisema tusiangalie ugeni peke yake, tutengeneze na sisi sekta binafsi ya ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, katika kufanya hivyo kwa sasa Mtanzania na yeye anaweza kuchukua mradi mkubwa na yeye ndiyo akatoa *sub-contract* kwa wale wageni na kama atahitaji

wawe wengi kiasi gani ama utaalamu kiasi gani na anaweza hata akaajiri wataalamu kutoka nje ili kuweza kuhakikisha kwamba na sisi tunakuwa na makampuni ya ndani yanayoweza kufanya shughuli kubwa na yakafanya kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, tumeona uamuzi huo wa Mheshimiwa Rais katika kazi zilizofanyika za hivi karibuni, madaraja mengi kati ya yale madaraja takribani 81 yaliyojengwa nchi nzima kufuatia uharibifu ule uliojitokeza. Tuna madaraja mengi yamejengwa na tena yamejengwa kwa ubora na yamejengwa na wakandarasi wazawa. Kwa hiyo, hili ndio eneo ambalo tumeliwekea kwenye sheria tukiwa tunalenga kujenga nguvu ya uchumi inayomilikiwa na Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu uwekezaji hilo lipo wazi kwa mtu yeyote kuja kuwekeza na tunaamini kwamba ni jambo ambalo linachangia kwenye uchumi wetu. Hili la kazi za mikataba; ujenzi, miradi ya barabara, ya maji na mingineyo, tulikuwa tunaiepusha nchi kwamba miradi mingine tumechukua fedha za kukopa halafu tunawapa wakandarasi wageni, wanapata *supernormal profit* (faida na ya juu) na baada ya hapo wanatuachia sisi kama nchi tukishughulikia mikopo ama madeni ambayo tumekopa kutekeleza miradi hiyo, wao wakiwa wameshachukua faida na wakati uwezo wa Watanzania ambao wangeweza kufanya kwa kiwango kilekile upo. Kwa hiyo, hilo ndilo ambalo tumelitofautisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa nafasi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, nakushukuru sana kwa majibu mazuri, ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaendelea, juzi kulikuwa na Fainali za *Under 17,* Mheshimiwa Rais alitoa usafiri wa ndege na hamasa ili timu yetu ipate ushindi. Bahati mbaya mpira una matokeo machungu, hatukufanikiwa.

Waheshimiwa Wabunge, lakini pamoja na hayo kuna Wabunge walijiunga na msafara huu kwenda Morocco.

Wabunge hawa wote hawana vibali vya Ofisi ya Spika kutoka nje ya nchi. Kwa maana hiyo, natoa maelekezo kwa Katibu wa Bunge, Wabunge wote waliosafiri bila Kibali cha Spika au Ofisi ya Spika waandikiwe barua za kujieleza kwa nini wamevunja Kanuni za Kibunge na kutoka nje ya nchi bila Kibali cha Ofisi ya Spika. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pamoja na nia nje iliyokuwepo, taratibu za Kibunge lazima zifuatwe. *(Makofi)*

Katibu wa Bunge, wape siku nne kuleta majibu yao na pale watakaposhindwa, hatua za kikanuni na za kinidhamu zichukuliwe dhidi ya Wabunge wote waliokwenda Morocco bila Kibali cha Ofisi ya Spika. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tuna kundi lingine la utoro ndani ya Bunge, mtu anakuja asubuhi, ana-*verify,* anaondoka anakwenda nyumbani kwake, anakuja jioni ana-*verify,* anaondoka anakwenda nyumbani kwake, huu ni utoro vilevile. *(Makofi)*

Kuna wengine wanachukua nafasi ya kutokuwepo, lakini wenzao kuwasainia kwenye karatasi zetu za manjano kujifanya na wao wapo. Yule anayesaini tunamjua, wanafahamika; na yule anayesainiwa anafahamika vilevile kuwa ni mtoro, hao nao tutawachukulia hatua za kisheria na za kikanuni. *(Makofi)*

Kuna Wabunge wengine yote hayo hawafanyi, lakini ndani ya Bunge hawapo, huo ndiyo utoro uliokithiri, kudharau Mamlaka ya Ofisi ya Spika na kudharau wananchi waliotuleta humu ndani. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kuanzia Jumatatu hatutegemei hayo kufanyika tena na Ofisi ya Katibu ina uwezo wa kum-*trace* kila Mbunge alipo kwa *signal* za simu. Ukiwa Songea, Katibu anajua huyu yupo Songea, na hata ukizima simu yako, simu za sasa hivi bado zina *signals. (Makofi)*

Kuna Mbunge ameomba Kibali cha Spika anakwenda jimboni, lakini anakwenda nje ya nchi na sijui anavuka vipi

kwenye viwanja vyetu vya ndege kwenda nje ya nchi bila Vibali vya Spika. Hata ukiwa nje ya nchi Ofisi ya Katibu ina uwezo wa kujua upo nchi gani kwa *signal* ya simu yako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano anatusaidia ku-*trace* watu, tunayo orodha kubwa sana. Tunafanya utu na heshima na hivi sasa inaelekea utovu wa mahudhurio ya Bunge umezidi sana.

Mheshimiwa *Chief Whip* moja ya majukumu yako ni haya, kuhakikisha nidhamu ndani ya Bunge siyo kwenye mijadala tu, pamoja na mahudhurio ya Wabunge ndani ya Bunge. Nikuombe sana, najua Mawaziri mna vibali vyenu maalumu, lakini Mheshimiwa Waziri Mkuu haipendezi, Waziri ana ziara na Naibu Waziri ana ziara kipindi hicho hicho. Wapeane zamu, mmoja abaki ndani na mmoja aende kwenye ziara, na haya maelekezo yalishatolewa siku nyingi na Mheshimiwa Rais, mahudhurio ndani ya Bunge ya Mawaziri na ya Wabunge. *(Makofi)*

Kwa hiyo, upande wa Mawaziri, Mheshimiwa Waziri Mkuu hili ni la kwako wewe pamoja na mamlaka inayotoa vibali, lakini tungependa sana kuona Naibu kama hayupo, Waziri wake yupo au kama Waziri hayupo, Naibu wake awepo Bungeni asikilize mijadala ya Wabunge kuweza kujibu na kuwasaidia wananchi wetu kuondokana na kero zilizokuwepo. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:** Maswali ya Kawaida.

## MASWALI NA MAJIBU

**SPIKA:** Maswali kwa Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Salehe Mbwana Mhando.

Na. 508

**Fedha za Awamu ya Pili kwa Ajili ya Kukamilisha Vituo vya Afya**

**MHE. SALEHE M. MHANDO** aliuliza: -

Je, lini Serikali itapeleka fedha za awamu ya pili kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa Vituo vya Afya vya Vuju, Mswaki na Negero katika Jimbo la Kilindi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Salehe Mbwana Mhando, Mbunge wa Jimbo la Kilindi, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kutoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya vya katika kata za kimkakati kote nchini. Katika kipindi cha miaka mitano Serikali imejenga jumla ya vituo vya afya 487 vikiwemo Vituo vya Afya vya Vuju, Mswaki na Negero katika Halmashauri ya Wilaya ya Kilindi.

Mheshimiwa Spika, Serikali imefanya tathmini na kuainisha jumla ya vituo vya afya 364 vyenye upungufu wa miundombinu muhimu. Aidha, vituo 111 vimetengewa bajeti ya shilingi bilioni 23.37 katika mwaka 2026/2027 kwa ajili ya ukamilishaji ikiwemo Halmashauri ya Wilaya ya Kilindi ambayo imetengewa shilingi milioni 200 kukamilisha Vituo vya Afya Vuju na Mswaki. Aidha, Kituo cha Afya Negero ni kati ya Vituo vya Afya 120 vya kimkakati vilivyopokea shilingi milioni 250 kupitia bejeti ya nyongeza ya mwaka wa fedha 2024/2025. Ujenzi umehusisha jengo la kuhudumia wagonjwa wa nje *(OPD),* choo cha nje na kichomea taka na ujenzi upo hatua ya ukamilishaji.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutenga fedha kwa awamu na kukamilisha ujenzi wa miundombinu ya vituo vya afya ili viweze kutoa huduma muhimu ikiwemo huduma za upasuaji wa dharura kwa akinamama wajawazito.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Mhando.

Waheshimiwa Wabunge wengine naomba mzime *microphones* zenu.

Mheshimiwa Mhando, tayari.

**MHE. SALEHE M. MHANDO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana na nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, pamoja na majibu hayo naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Kilindi kupitia mapato yake ya ndani imeanza ujenzi wa vituo vya afya katika Kata ya Kilindi Asilia, Kata ya Masagalu pamoja na ujenzi wa jengo la wagonjwa wa nje katika Kituo cha Afya cha Kwedibomu.

Je, Wizara ina mpango gani wa kupeleka fedha kwa ajili ya kwenda kuunga mkono jitihada za Halmashauri ya Kilindi ili kukamilisha ujenzi wa vituo hivyo ili viweze kutoa huduma kwa wananchi?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; mwaka wa fedha 2021 Kituo cha Afya cha Vuju, Kata ya Tunguli kilipokea jumla ya shilingi milioni 400 kwa ajili ya ujenzi wa majengo matatu; jengo la wagonjwa wa nje, jengo la wodi ya mama na mtoto, pamoja na jengo la upasuaji. Changamoto iliyopo kwenye utekelezaji wa mradi ule ni jengo moja tu la wagonjwa wa nje liliweza kukamilika na majengo mawili; jengo la mama na mtoto pamoja na jengo la upasuaji hayajakamilika mpaka hivi tunavyoongea zaidi ya miaka mitano hayafanyi kazi kabisa. Hali kadhalika Kituo cha Afya Kwediboma kilipelekewa jumla ya shilingi milioni 300 kwa ajili ya

ujenzi wa majengo matatu na majengo hayo hayajakamilika mpaka hivi tunavyoongea.

Mheshimiwa Spika, je, Wizara ina utaratibu gani wa ufuatiliaji na uchukuaji wa hatua kwa miradi na vituo vya afya vinavyopelekewa fedha na majengo yake kutokukamilika kwa muda mrefu kiasi hiki na inaonekana kuna sababu za ubadhirifu?

**SPIKA:** Mheshimiwa uliza swali lako, acha maelezo.

**MHE. SALEHE M. MHANDO:** Mheshimiwa Spika, kutokana na hali hiyo Wizara inachukua hatua gani za ufuatiliaji na kuchukua hatua katika vituo hivyo ambavyo majengo yake hayajakamilika kwa muda mrefu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali madogo mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge Mhando, Mbunge wa Jimbo la Kilindi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza ni utaratibu wa halmashauri kutenga fedha mapato ya ndani kwa ajili ya kuendelea kujenga miundombinu katika vituo vyetu vya afya, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI itaendelea kutenga bajeti ili kuhakikisha vile vituo ambavyo tayari halmashauri imevianzisha kuweza kuvisaidia kuweza kukamilisha vituo hivyo.

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali dogo la nyongeza la pili la hatua ya ufuatiliaji katika vile vituo vya afya ambavyo tayari Serikali ilielekeza fedha.

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa ufuatiliaji upo Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI, tuna timu Kitengo Maalum cha Ufuatiliaji na nimuelekeze Mkurugenzi wa Halmashauri aweze kufuatilia vituo hivyo ambavyo Mheshimiwa Mbunge amevianisha hapa na

atuletee taarifa Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI ili tuweze kuchukua hatua stahiki.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge ushirikiano dhati ili kuhakikisha huduma lengwa za kuwahudumia watu wetu katika Jimbo la Kilindi zinafikiwa.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Waheshimiwa kutokana na wageni kuwa wengi na Bunge letu lina wageni wengi wako nje na ndani, naomba kuwatangaza wageni wa sasa hivi ili wakishatambulishwa wawapishe wenzao na wao waje kushuhudia Bunge likifanya kazi.

Wageni waliopo Bungeni asubuhi hii: wapo wageni wa Waheshimiwa Wabunge; wageni watatu wa Mheshimiwa Hamis Mohamed Mwinjuma, Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, ambao hawa ni wafanyabiashara wa Kampuni ya *Aurora Scents* kutoka jijini Dar es Salaam, karibuni. *(Makofi)*

Wageni wa Mheshimiwa Ng'wasi Damas Kamani, Naibu Waziri Mifugo na Uvuvi; Ndugu James Kashindye, mpigakura wake na Mjumbe wa Mkutano Mkuu wa UVCCM, Mkoa wa Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Devotha Daniel Mburarugaba ambaye ni Ndugu Alphonce Kagaruki, mkulima kutoka Mkoa wa Kagera. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Patali Shida Patali, wafanyabiashara na wadau wa zao la pareto kutoka Jijini Mbeya. *(Makofi)*

Wageni 14 wa Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, madaktari na wauguzi wa Hospitali ya Rufaa ya *General* ya Jijini Dodoma wakiongozwa na Dkt. Mukhsin Chikota, mtoto wa Mheshimiwa. *(Makofi)*

Dkt. Mukhsin Chikota simama peke yako tukuone. Hongera sana. Huyu ndiyo mtoto wa Mheshimiwa Mbunge Chikota. *(Makofi)*

Wageni 24 wa Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam *(UDSM)*. *(Makofi)*

Wageni 39 wa Mheshimiwa Anna Richard Lupembe ambao ni wanafunzi na walimu kutoka Chuo cha Ufundi Dodoma. *(Makofi)*

Wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo: wapo wanafunzi 155 na walimu 16 wa Shule ya Awali na Msingi ya Libermann ya Jijini Dar es Salaam. Karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa tunaendelea. Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga.

Waheshimiwa Wabunge ambao mpo kwenye foleni ya maswali ya nyongeza naomba mzime *microphones* zenu.

Na. 509

**Ujenzi wa Barabara kwa Kiwango cha Lami Vwawa-Isalalo**

**MHE. JAPHET N. HASUNGA** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami kutoka Vwawa – Londoni – Msia hadi Isalalo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa Barabara ya Vwawa – Londoni mpaka Msia yenye urefu kilometa 13.7 ambayo inahudumiwa na *TARURA* na kutoka Msia hadi Isalalo yenye urefu wa kilometa 20.5 inahudumiwa na *TANROADS*.

Kutokana na umuhimu wa Barabara ya Vwawa – Londoni hadi Msia, imeingizwa kwenye Mradi wa *TACTIC* unaofadhiliwa na Benki ya Dunia. Kwa awamu ya kwanza barabara hiyo itajengwa kwa urefu wa kilometa 2.0 kwa kiwango cha lami kuanzia Vwawa.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu wa barabara ya Vwawa – Londoni mpaka Msia yenye urefu wa kilometa 13.7 iliyopo katika Wilaya ya Mbozi, Serikali imeendelea kuihudumia, ambapo katika mwaka wa fedha 2023/2024, Serikali ilitenga jumla ya shilingi milioni 17.65 kupitia Mfuko wa Barabara *(Road Fund)* kwa ajili ya kuchonga barabara hiyo kwa urefu wa kilometa 6.0 na kuzibua makalvati pamoja na mifereji ya maji ya mvua.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Serikali imetenga jumla ya shilingi milioni 36.69 kupitia fedha za Mfuko wa Barabara *(Road Fund)* kwa ajili ya kuchonga barabara kwa urefu wa kilometa 6.14, na kujenga *box culvert* mistari miwili.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuzihudumia barabara katika Jimbo la Vwawa ikiwemo Barabara ya Vwawa-Londoni-Msia ili ziweze kupitika muda wote.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hasunga.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana na kwanza naishukuru Serikali kwa majibu mazuri ambayo yametolewa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa katika maeneo ambayo Serikali tayari imetenga shilingi milioni 17.6 kwa ajili ya ujenzi wa mifereji pamoja na makalvati yalijengwa chini ya kiwango, mifereji iko juu barabara iko chini, kwa hiyo, maji yanarudi kwenye barabara badala ya kutoka nje. Je, Serikali iko tayari sasa kuongeza usimamizi ili mifereji hiyo ijengwe kwa kiwango kinachotakiwa?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, tunashukuru kwa mpango wa kutujengea kwamba mtajenga kilometa mbili kwenye Mradi ule wa *TACTIC* kilometa mbili, lakini kilometa mbili hazitufikishi kwenye eneo ambalo ni baya sana la Mto Nkana ambalo liko karibu kilometa nne, je, Serikali iko tayari kuongeza kilometa badala ya kuwa mbili ziwe tano ili tufike eneo ambalo ni baya sana wakati wa masika ili liweze kupitika?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali madogo ya nyongeza ya Mheshimiwa Hasunga, Mbunge wa Jimbo la Vwawa, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwanza nakubaliana naye kwamba maeneo ambayo kuna usimamizi ambao si thabiti unaleta changamoto ya ukamilishaji wa miradi hii. Kupitia Bunge lako Tukufu na kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, nimuelekeze Meneja wa *TARURA* Mkoa afike eneo ambalo Mheshimiwa Mbunge ameliainisha ili kuweza kufanya tathmini na kuona uhalisia wa jambo ambalo Mheshimiwa Mbunge ameliwasilisha hapa na Serikali tuweze kuchukua hatua.

Mheshimiwa Spika, swali la pili nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwa kuwa barabara hii sasa tumeihamishia *TACTIC*, fedha hizi za uhakika zinazotoka *World Bank*, tuendelee kuwa na subira kwa ujenzi wa kuanza na hizi kilometa mbili na tutaendelea kutenga fedha kuhakikisha Mheshimiwa Mbunge tunakamilisha adhma ya kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami na ili iweze kutoa huduma iliyokusudiwa kwa wananchi wa jimbo la Vwawa.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Alan Thomas, jiandae Mheshimiwa Ndumbaro.

**MHE. ALAN T. MVANO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, katika Wilaya ya Kakonko tunashukuru sana Serikali kwa kutujengea kilometa tatu za lami kuelekea hospitali ya wilaya, ukiacha barabara hiyo mtandao wa lami katika Mji wa Kakonko ambao ndiyo makao makuu ya wilaya tuna meta 950 peke yake. Kwa kuwa moja ya ahadi ya kiongozi wa nchi ilikuwa ni kuongeza mtandao wa barabara za lami, ni upi mpango wa Serikali kuhakikisha sasa Makao Makuu ya Wilaya ya Kakonko yanaongezewa barabara kwa kiwango cha lami?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Alan, Mbunge wa Jimbo la Kakonko na nimpongeze kwa kuendelea kuwapambania wanajimbo la Kakonko na wanajimbo wanafahamu Mbunge wao kwa namna gani anavyowasilisha changamoto za jimbo na sisi kama Serikali Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tutaendelea kutenga bajeti na kuhakikisha tunafanya ujenzi katika barabara hizo ambazo Mheshimiwa Mbunge umeziainisha.

Mheshimiwa Spika, ni mpango wa Serikali kila halmashauri na makao makuu ya halmashauri kuendelea kujenga barabara hizi kwa kiwango cha lami angalau kwa awamu kwa kila mwaka ili kuhakikisha halmashauri zetu zinapata huduma hii na zinakuwa *smart*. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge Serikali itaendelea kumpa ushirikiano kuhakikisha kwamba tunajenga barabara hizo na zinatoa huduma iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Dkt. Ndumbaro, jiandae Mheshimiwa *Engineer* Kija.

**MHE. DKT. DAMAS D. NDUMBARO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, barabara ya kutoka Kata ya Mletele kwenda Kata ya Mshangano ndio mkombozi katika Manispaa ya Songea kipindi cha masika wakati barabara kubwa inajifunga.

Je, ni lini sasa Serikali itajenga barabara hii ya kutoka Kata ya Mletele kwenda Kata Mshangano kwa kiwango cha lami?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Ndumbaro kuwa mpango wa Serikali ni kuhakikisha tunajenga barabara hizi kwa kiwango cha lami, barabara ambayo ameiainisha; kwanza tunaanza na moramu, changarawe ili kuweza kuziweka katika huduma bora na ziendelee kutoa huduma kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tutaendelea kumpa ushirikiano kuhakikisha kwamba tunazijenga barabara hizi ili ziweze kupitika masika na kiangazi na zitoe huduma ambayo Serikali imekusudia.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa *Engineer* Kija.

**MHE. KIJA L. NTEMI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Mheshimiwa Waziri katika Mji wa Katoro barabara nyingi bado zina changamoto ya kupitika. Je, ni lini sasa Serikali itaingiza Mji wa Katoro katika mfumo wa *TACTIC* ili uweze kujengwa na kutengenezwa kwa haraka ili kuwapunguzia wananchi wa Katoro adha ya barabara mbovu ambazo zipo katika Mji wa Katoro?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kija Limbu Ntemi, Mbunge wa Jimbo la Katoro na nimpongeze kwa namna ambavyo anaendelea kufuatilia changamoto za Jimbo la Katoro.

Mheshimiwa Spika, Katoro ipo chini ya Mamlaka ya Mji Mdogo na huwa inaendelea kupokea zile barabara ambazo ni za kuendeleza Mamlaka ya Miji Midogo, lakini nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutaendelea kutenga bajeti kuhakikisha kwamba, mji wetu wa Katoro na ongezeko kubwa la watu na aina ya jiografia kwa sababu ya mmomonyoko wa ardhi, kwa sababu ya mvua zinazoendelea kunyesha, tutaendelea kuufanya mji wetu uwe bora na uweze kupitika nyakati zote za masika na kiangazi, ili sasa ile huduma ambayo imekusudiwa ya kutoa huduma bora za barabara Jimbo la Katoro liweze kupitika maeneo yote.

Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Kija Limbu Ntemi, Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI tutaendelea kumpa ushirikiano na kujenga barabara hizo. Naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Daniel Awack, kwa niaba yake Mheshimiwa Kakoso.

Na. 510

**Upungufu wa Vyumba ya Madarasa Shule ya Matala na Lositete – Karatu**

**MHE. MOSHI S. KAKOSO K.n.y. MHE. DANIEL A. TLEMAI** aliuliza:-

Je, lini Serikali itatatua changamoto ya upungufu wa vyumba vya madarasa katika Shule ya Matala na Lositete Karatu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Daniel Awack Tlemai, Mbunge wa Jimbo la Karatu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikijenga shule mpya za sekondari, kuongeza miundombinu katika shule zilizopo ili kuendana na ongezeko la wanafunzi.

Mheshimiwa Spika, kati ya mwaka 2021/2022 hadi 2025/2026 Serikali imepeleka jumla ya shilingi bilioni 1.63 kwa ajili ya ujenzi wa shule mpya tatu za sekondari, madarasa 116, maabara 17, matundu ya vyoo 182, mabweni 11 na nyumba za walimu 10 zilipokea jumla ya shilingi milioni 79.

Mheshimiwa Spika, narudia, kati ya mwaka 2021/2022 hadi 2025/2026 Serikali imepeleka jumla ya shilingi bilioni 1.63 kwa ajili ya ujenzi wa shule mpya tatu za sekondari, madarasa 116, maabara 17, matundu ya vyoo 182, mabweni 11 na nyumba za walimu 10 katika Shule za Sekondari za Halmashauri ya Karatu. Shule za Matala na Lositete zilipokea jumla ya shilingi 79,000,000 kwa ajili ya ujenzi wa darasa moja na matundu ya vyoo mawili katika Shule ya Matala na ukamilishaji wa nyumba moja ya mwalimu na chumba kimoja cha darasa katika Shule ya Lositete.

Mheshimiwa Spika, mwaka wa fedha 2026/2027 Serikali imetenga jumla ya shilingi milioni 452.6 kwa ajili ya ujenzi wa matundu ya vyoo 30, maabara nne, darasa moja, nyumba moja ya mwalimu na vitanda 120 katika Shule za Sekondari ya Wilaya ya Halmashauri ya Karatu. Shule za Matala na Lositete zitapokea jumla ya shilingi 145,000,000 kwa ajili ya ujenzi wa maabara moja katika Shule ya Matala na maabara moja na darasa moja katika Shule ya Lositete.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa shule mpya na kuongeza miundombinu katika shule zilizopo ili kuendana na ongezeko la wanafunzi. Naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kakoso.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa juhudi zilizofanywa na Serikali zimeonekana na tunashukuru kwa kazi kubwa ambayo imefanyika, lakini bado kuna uhitaji mkubwa wa tatizo la vyumba vya madarasa, sambamba na ukosefu wa nyumba za walimu. Nini tamko la Serikali kumaliza tatizo hilo?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika ina shule ambazo zina tatizo kubwa na upungufu mkubwa wa madawati na vyumba vya madarasa kwenye Kata ya Kapalamsenga na Kata ya Kamsanga. Ni lini Serikali itapeleka fedha hizo kwa ajili ya kutatua kero ya uhaba wa vyumba vya madarasa? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF)**: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali madogo ya nyongeza yaliyoulizwa na Mheshimiwa Mbunge Kakoso kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kutenga fedha na imeendelea kuainisha mipango thabiti kwa ajili ya ujenzi wa madarasa pamoja na nyumba za watumishi. Katika Bunge lako Tukufu nilikwishaeleza mpango mahsusi ambao tulienda nao pale Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI kuhakikisha kwamba sasa tunaenda kuanza kwa awamu ujenzi wa nyumba za watumishi 2,000 ambazo tutashirikisha sekta binafsi ili kuhakikisha kwamba nyumba hizi tunazikamilisha kwa wakati na watumishi wetu wapate nyumba hizi, ili waweze kufundisha watoto wetu kwa utulivu.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya madawati na kujenga madarasa, na mpango uliopo, madarasa ya sasa yakijengwa lazima yawe na madawati angalau 45 ili kuhakikisha kwamba watoto wetu wanaanza kupata huduma.

Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa Serikali itaendelea kufanya juhudi hizi ili kuona kwamba tunajenga madarasa

ambayo yanakuwa na madawati ili watoto wetu wapate mahali salama pa kujifunzia. Naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Bakari Shingo.

**MHE. BAKARI B. SHINGO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote nitoe shukrani sana kwa ufafanuzi kutoka TAMISEMI juu ya kero ya michango shuleni na nina uhakika sasa, tunaenda kumaliza karaha ya michango isiyokuwa na maana ambayo mingi imekuwa inaleta lawama kwa Serikali yetu.

Mheshimiwa Spika, nilitaka nifahamu mpango wa Serikali baada ya mvua kuharibu barabara zetu huko mitaani, hasa katika Jimbo langu la Ukonga. Ni lini sasa Serikali wataanza kusambaza kifusi kwa ajili ya kujaza hizo barabara hasa za kule Ulongoni A, Ulongoni B, Barabara ya Mwembe Supu kuelekea kule Mwembe Samaki. Naomba Mheshimiwa Waziri atueleze kwamba karaha hii inakuwaje ili tuweze kuondokana na mashimo ambayo…

**SPIKA:** Mheshimiwa Shingo swali lako umeuliza la barabara siyo?

**MHE. BAKARI B. SHINGO:** Mheshimiwa Spika, naam.

**SPIKA:** Swali lako ni kifusi cha barabara?

**MHE. BAKARI B. SHINGO:** Mheshimiwa Spika, kifusi kwenye barabara zetu ambazo ziko chini…

**SPIKA:** Swali la msingi ni vyumba vya madarasa, lakini Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa heshima ya wananchi mjibu. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF):** Mheshimiwa Spika,

ahsante sana, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Shingo kama ifuatavyo:-

Kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa namna ambavyo amekiri, Serikali tumetoa maelekezo mahususi kuhusiana na michango holela shuleni; lakini suala lake la barabara, kwanza nimwelekeza Meneja wa *TARURA* Wilaya, afike eneo ambalo Mheshimiwa Mbunge ameainisha na achukue hatua za dharura kuweza kusambaza vifusi hivi, ili wananchi waendelee kupata huduma stahiki. Naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Tinnar Chenge.

**MHE. TINNAR A. CHENGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa shule ya Sekondari ya Wasichana ya Simiyu ina wanafunzi ambao wana ulemavu, je, ni lini Serikali itatatua changamoto ya miundombinu wezeshi ili wanafunzi hawa, waweze kwenda darasani na hasa katika kipindi cha mvua?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Tinnar Chenge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza miundombinu ya shule na miundombinu inayotoa huduma katika jamii zetu, yote imejengwa ili iweze ku-*accommodate* walemavu katika jamii zetu. Kwa hiyo, nimwelekeze mkurugenzi, afike katika shule ambayo Mheshimiwa Mbunge ameiainisha, ili kwanza kujiridhisha kama kweli miundombinu haipo; na kama haipo achukue hatua za dharura kuweza kuweka miundombinu hii, ili vijana wetu walemavu wanaopata elimu katika shule hizi waweze kupata elimu bila changamoto yoyote. Naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Hawa Mwaifunga.

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniona. Shule ya msingi iliyoko katika Kata ya Mtakilwa, Jimbo la Tabora Mjini, ina upungufu mkubwa sana wa madarasa. Kuna madarasa matano peke yake, hivyo kupelekea wanafunzi kusoma kwa awamu. Ni nini mpango wa Serikali kuhakikisha kwamba wanaongeza madarasa ili wanafunzi waweze kusoma kila mwanafunzi na darasa ambalo anatakiwa awepo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Hawa Mwaifunga, Mbunge wa Jimbo la Tabora Mjini na Mjumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Hawa Mwaifunga, Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI tayari imeshaandaa mpango wa kuhakikisha kwamba shule hii tunakwenda kuiongezea madarasa, ili wanafaunzi wetu waweze kusoma bila changamoto yoyote. Naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Zuberi Mfaume.

**MHE. ZUBERI Y. MFAUME:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Morogoro Kusini lina kata 17 na takribani katika kila kata tayari wananchi wameshajenga maboma ya madarasa na sasa wanasubiri pesa za kumalizia kutoka Serikalini.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri, ni lini sasa mtatuingizia pesa ili tuweze kumaliza vyumba hivyo vya madarasa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mfaume, Mbunge wa Jimbo la Morogoro.

Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge pamoja na wananchi kwa kuweka nguvu zao na kwenda kujenga maboma hayo na ni maelekezo mahususi ya Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI kwamba kabla ya kuanza miradi mipya, tuhakikishe maboma yote tunayakamilisha na yanatoa huduma tarajiwa.

Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa jimbo, tunakwenda kukamilisha maboma haya ili kuhakikisha kwamba yanaanza kutoa huduma kwa wakati na tukielekea mwaka 2028 ambapo tutapokea *double cohort* ya wanafunzi darasa la sita na la saba wote watamaliza kwa pamoja, kwa hiyo, ni lazima tuhakikishe miundombinu hii tunaikamilisha kwa wakati ili ikatoe huduma kwa wananchi wetu. Naomba kuwsilisha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Getere.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Shule ya Msingi Malambeka, Shule ya Msingi za Mkomalilo A na Mkomalilo B, Shule ya Msingi ya Nachilo B zote zimebomoka na nyingine watoto sasa hivi wanakaa chini. Lini Serikali itaenda kurekebisha madarasa ya shule hizo ili watoto wasome?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Getere kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, nipokee kama ombi kutoka kwa Mheshimiwa Getere na sisi Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI niwaelekeze wataalamu wetu waweze kufuatilia takwimu halisi za

shule hizo na changamoto ambazo zimejitokeza, ambazo Mheshimiwa Mbunge ameziwasilisha, ili Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI tuweze kuchukua hatua za dharura kuhakikisha kwamba tunaweka mazingira bora ya kujifunzi ya wanafunzi wetu. Naomba kuwasilisha

**SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Twaha Said Mwakioja.

Na. 511

**Ukarabati wa Madarasa Chakavu – Mkinga**

**MHE. TWAHA S. MWAKIOJA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itakarabati madarasa chakavu na kujenga madarasa mapya katika Shule za Msingi Jimbo la Mkinga?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Twaha Said Mwakioja, Mbunge wa Jimbo la Mkinga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kufanya ukarabati wa shule katika Wilaya ya Mkinga ambapo katika mwaka wa fedha 2021/2022 mpaka kufikia mwaka 2025/2026, Serikali imepeleka jumla ya shilingi bilioni 2.78 katika Wilaya ya Mkinga kwa ajili ya ujenzi wa shule mbili mpya za msingi, madarasa 82 katika shule 35 chakavu za msingi na ukarabati wa shule tatu chakavu za msingi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2026/2027 Serikali imetenga jumla ya shilingi milioni 275.2 kwa ajili ya ujenzi wa madarasa matatu, matundu ya vyoo 94 katika shule 19 za msingi katika Jimbo la Mkinga.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya kujenga madarasa na kukarabati shule za msingi chakavu nchini zikiwemo shule za Jimbo la Mkinga. Naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwakioja.

Waheshimiwa Wabunge, punguzeni maongezi na wengine zimeni *microphones* zenu.

**MHE. TWAHA S. MWAKIOJA:** Mheshimiwa Spika, kwanza niishukuru Serikali kwa majibu mazuri na juhudi ambazo imezionesha kwa kipindi chote.

Mheshimiwa Spika, nimepata bahati ya kuzitembelea takribani shule zote za sekondari na msingi katika jimbo ninaloliongoza la Mkinga, kwa kweli hali ya shule hizi haiko vizuri hususan shule za msingi. Zipo shule zinavuja, zipo shule sakafu ni tifutifu kama vile uwanja wa mpira; na zipo kuta zinataka kuanguka.

Je, kutokana na hali hii, ni upi sasa mkakati wa Serikali wa kuhakikisha inaongeza fedha ambazo inazitenga ili kuondokana na adha hii; kwa sababu kuna baadhi ya madarasa nimeingia, watoto wanajitenga, hawa darasa la tano, hawa darasa la sita. Darasa moja wapo humo humo wanasoma pamoja. Ni upi mkakati wa Serikali kuongeza fedha ili kuhakikisha kwamba inaondokana na adha hii na kuweza kutoa elimu iliyo bora?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; nimwombe Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI ikimpendeza tuongozane naye ili akaone adha ya shule na miundombinu iliyopo katika Jimbo la Mkinga. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba kujibu maswali madogo ya nyongeza ya

Mheshimiwa Twaha Said Mwaikoja, Mbunge wa Jimbo la Mkinga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI tuliwasilisha katika bajeti katika Bunge lako hili Tukufu kwamba tunao mradi unaoitwa *School Infrastructure Facelifting Programme (SIFA)*. Mradi huu unakwenda kuboresha shule hizi hasa zile kongwe na Bunge lako hili Tukufu lilipitisha bajeti ile na tutakwenda kuhakikisha kwamba tunaongeza fedha katika shule ambazo, kwanza ni chakavu na zile za muda mrefu na zile zenye mahitaji muhimu. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa tutahakikisha tunaongeza fedha katika maeneo yote aliyoyataja ili kuhakikisha tunaboresha miundombinu ya elimu katika jimbo lake.

Mheshimiwa Spika, swali la pili kuhusu ziara; Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI tumeendelea kufanya ziara ambazo zinaongozwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu na tatatenga ratiba mimi na Mheshimiwa Mbunge ili tuweze kufika jimboni kuangalia miundombinu, siyo tu ya elimu hata maeneo mengine mbalimbali ili kuhakikisha kwamba ile azma ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kuacha tabasamu kwa Watanzania inakwenda kutekelezwa. Naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Neema Mwandabila.

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, katika mkoa wangu wa Songwe kuna maboma mengi katika shule za msingi yalijengwa ni zaidi ya miaka kumi ambayo sasa nayo yameshapata uchakavu.

Sasa nataka kufahamu je, Serikali haioni kwa kuyaacha maboma hayo muda mrefu inawaumiza wananchi ambao walijitolea kipato chao kuweza kujenga maboma hayo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF):** Mheshimiwa Spika,

naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Neema kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza Serikali inatoa pongezi kwa nguvu kubwa za wananchi, jitihada ambazo wananchi wameweka kujenga maboma hayo na pili, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI imeendelea kufanya tathmini, kuna yale maboma ambayo yanaweza yakamaliziwa ambayo bado yapo ndani ya ubora, lakini kuna yale maboma ambayo tayari yameshaharibika zaidi, hatutaweza kuyamalizia. Yale ambayo yapo ndani ya ubora tutaendelea kuyafanyia kazi, tutaendelea kutenga bajeti kuhakikisha kwamba tunayakamilisha, ili yaweze kutoa huduma katika maeneo ambayo Mheshimiwa Mbunge ameyaainisha. Naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kiswaga.

**MHE. JACKSON G. KISWAGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi; je, Serikali imeweka makakati gani kwenye bajeti hii ili ukarabati majengo ya shule za msingi ambayo yamechakaa sana ya shule kongwe? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kiswaga kama alivyoliuliza. Kama ambavyo nimekwishajibu kwenye majibu ya maswali madogo ya nyongeza, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI tunao mradi mkakati wa *SIFA;* mradi huu unatakiwa kwenda kuboresha shule zote chakavu kongwe nchini, ili kuweza kutoa huduma bora na kuzirejesha kwa maana ya kwamba zianze kuendana na usasa ambao utatoa huduma bora ya elimu kwa wanafunzi wetu. Naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mafuwe.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Spika, katika Jimbo la Hai kuna shule nyingi chakavu na tumeshawasilisha

andiko maalum TAMISEMI. Wakati tukiwa tunasubiria, hivi sasa mvua zinanyesha na maji yanaingia ndani, watoto wanashindwa kupata kuendelea na masomo. Shule ya Mkosaringe, Lyamungo, Shirimatunda, Rowu, Kisheri, Nkwamakuu, Tindigani, Waramu, Sereng na Shirimatunda.

Je, Serikali ina mpango gani sasa wa dharura kuhakikisha shule hizi zinafanyiwa ukarabati ili watoto waweze kuendelea na masomo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge kwa maana ya kwamba, anafuatilia, anatubana TAMISEMI kuhakikisha ya kwamba tunapeleka miundombinu stahiki na kwa wakati katika shule ambazo amezitaja.

Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza, jimbo hili lina shule kongwe kwa maana ya kwamba lilipata shule miaka ya nyuma sana. Kwa hiyo, wao walianza kupata miundombinu hii kwa kipindi cha miaka ya nyuma. Kwa hiyo, sasa hivi wameingia katika eneo la uchakavu na Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI tayari tumekwisha weka andiko, mipango mkakati kuhakikisha kwamba tunakwenda kuziboresha shule hizi ili ziweze kutoa huduma kusudiwa.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa pamoja na wanajimbo la Hai kwamba tutaendelea kupeleka fedha kuhakikisha kwamba tunakamilisha miundombinu hii ya shule na kuweza kutoa elimu kusudiwa. Naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Kabati.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa shule za msingi za Nyanzwa, Ibumu, Ikula na Iramba ni shule chakavu mno katika wilaya yetu ya Kilolo, na niwapongeze Serikali kwamba ina mpango wa kuzikarabati shule kongwe zote ambazo zimechakaa sana.

Je, Serikali ipo tayari kutanzia katika wilaya yetu ya Kilolo kwa sababu zimechaka mno na ni magofu, watoto wanasoma kwenye mazingira magumu sana?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge Dkt. Kabati wa Jimbo la Kilolo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo nimekwishatoa majibu ya Serikali kwamba tuna mpango makakati wa kupitia shule zote kongwe nchini na kuhakikisha tunaziboresha ili ziendane na usasa na kutoa huduma kusudiwa.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge nikuhakikishie wanakilolo wamekusikia na sisi Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI tumelichukua hili kuhakikisha kwamba katika kutenga vipaumbele na Jimbo la Kilolo tuweze kulitengea fedha na kwenda kufanya ukarabati wa shule hizo chakavu. Naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea na Ofisi ya Raisi, Mipango na Uwekezaji, Mheshimiwa Thomas Kitima.

Na. 512

**Utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050**

**MHE. THOMAS M. KITIMA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itaanza utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. LAURENT D. LUSWETULA) K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, ahsante sana, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Mipango na Uwekezaji nami naomba kujibu swali la Mheshimiwa Thomas Mgonto Kitima, Mbunge wa Jimbo la Ikungi Mashariki:-

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Dira 2050 utaanza rasmi tarehe 01 Julai, 2026 kufuatia kufikia ukomo wa Dira ya Taifa ya Maendeleo yam waka 2025 tarehe 30 Juni, 2026. Utekelezaji huu ni baada ya kuzinduliwa kwa Dira 2050 tarehe 17 Julai, 2025 na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Serikali inaendelea kuandaa nyenzo mbalimbali za utekelezaji wa dira hiyo, zikiwemo: -

(i) Mpango wa Maendeleo wa Muda Mrefu *(Long Term Perspective Plan)*;

(ii) Mpango wa Nne wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano wa mwaka 2026/2027 hadi 2030/2031;

(iii) Mwongozo wa Kitaifa wa Ufuatiliaji na Tathmini ya Miradi ya Maendeleo;

(iv) Mwongozo wa Kitaifa wa Uidhinishaji wa Miradi ya Maendeleo; na

*(v)* Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Mwaka Mmoja wa 2026/2027 *(Annual Development Plan)*.

Mheshimiwa Spika, baada ya kukamilika kwa nyenzo hizo, Serikali itaanza utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 sanjari na kutoa elimu kwa umma kuhusu mfumo na utaratibu utakaotumika katika utekelezaji wa dira hiyo, pamoja na mipango ya maendeleo ya miaka mitano na ya mwaka mmoja. Aidha, utekelezaji wa nyenzo hizo utafuatiliwa na kupimwa kidijitali kupitia mfumo wa *e-Delivery* (Mfumo wa Kitaifa wa Usimamizi wa Mipango na Miradi ya Maendeleo) kwa lengo la kuimarisha ufanisi, uwajibikaji na upatikanaji wa taarifa na takwimu za utekelezaji kwa wakati halisi.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Kitima.

**MHE. THOMAS M. KITIMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa dira hii inasema kwamba itawahusisha wananchi wote, kwa maana uchumi jumuishi na tunapoenda kuianza tarehe 01 Julai, 2026. Wananchi watahusikaje kwa sababu hakuna elimu ambayo imetolewa kwa umma ambayo itawafanya wawe sehemu ya mpango huu na sio wasindikizaji. Je, ni lini Serikali itatoa elimu kwa wananchi wote kabla hatujaanza kutekeleza?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; ni kwa namna gani miradi ambayo itatumika kama *benchmark* ama miradi ya kielelezo tunapoanza kuitekeleza dira hii tutaanza nayo mwezi Julai, ili wakati tunaendelea basi tuwe tunafanyiana *assessment* kupitia hiyo miradi ambayo tunaenda kuanza kuitekeleza tutakapoanza kutekeleza dira hii?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. LAURENT D. LUSWETULA) K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, kwanza nipende kumpongeza sana Mbunge wa Ikungi Mashariki, Mheshimiwa Thomas Kitima,

kwa kuendelea kupambania sana wananchi wa jimbo hilo, lakini pia kama mjumbe makini katika Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti.

Mheshimiwa Spika, nikianza na swali la kwanza; niseme kabisa moja ya majukumu ya Wizara yetu ya Mipango na Uwekezaji kupitia Tume ya Taifa ya Mipango kwanza ni kuratibu na usimamizi wa uchumi, kupanga mipango ya maendeleo, pamoja na kutekeleza mipango ya maendeleo ambayo tayari imeshakwisha kuidhinishwa. Hii ni pamoja na kukusanya, kuchakata pamoja na kufanya tathmini ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ambayo tayari imeidhinishwa.

Mheshimiwa Spika, mimi niseme ni Naibu Waziri wa Fedha, na sisi kama Wizara ya Fedha, kwanza tumejidhatiti kuhakikisha kwamba Dira hii ya 2050 inatimizwa kwa 100%. Sisi tuko tayari kuhakikisha kwamba fedha ya aina yoyote ambayo inahitajika kulingana na mpango huu wa Dira ya 2050, tuko tayari kupeleka katika Wizara ya Mipango na Uwekezaji, kuhakikisha kwamba maono sasa ya mama yetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kuhakikisha kwamba uchumi wa nchi hii unafikia dola za Kimarekani trilioni moja ifikapo mwaka 2050, lakini pia wastani wa kipato cha mtu mmoja mmoja kufikia dola za Kimarekani 7,000 kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, kwa namna hiyo nimhakikishie kabisa Mheshimiwa Mbunge wa Ikungi Mashariki, sisi kama Wizara ya Fedha kwa kushirikiana na wenzetu wa Wizara ya Mipango na Uwekezaji, tuko tayari kuhakikisha kwamba mipango yote ambayo imo ndani ya Dira ya 2050 inatekelezwa bila kikwazo chochote kwa ukamilifu wake.

Mheshimiwa Spika, swali la pili ambalo ameuliza sasa ni kwa namna gani elimu kwa umma tunaenda kuifikisha huko. Kwanza niseme kabisa jambo hili la elimu kwa umma sio jambo la Serikali pekee yake, bali ni jukumu letu sisi kama Serikali, lakini pia na Wabunge wote ambapo tutakapokuwa tunakwenda kwenye majimbo yetu, ni lazima tuhakikishe ya kwamba tunatoa elimu

kwa umma ili umma sasa uelewe kwamba Dira hii ya 2050 imebeba maono gani.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, Dira ya Maendeleo ya miaka 25 kuanzia Julai 01, Dira ya Maendeleo 2050, kwanza na yenyewe kwa ukubwa wake, hatuwezi kuwakwepa sekta binafsi. Nazo tumezijumuisha kuhakikisha kwamba sekta binafsi zina-*play role* kubwa kutekeleza utekelezaji wa Ilani ya Dira ya Maendeleo 2050. Pia wenzetu wa Wizara ya Mipango, wana mpango mkakati mzuri sana wa kutoa elimu kwa umma kupitia *platform* mbalimbali ikiwemo makongamano, *social media* na vyombo vingine ambavyo vitahakikisha kwamba elimu ya utekelezaji wa Dira 2050 wananchi wanaielewa vizuri ili na wao waipokee kwa ajili ya utekelezaji wa dira hiyo.

Mheshimiwa Spika, ahsante na naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Faraji Nandala.

**MHE. FARAJI B. NANDALA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi ili nami niweze kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kundi la vijana ndio kundi lengwa katika utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025/2050 na Serikali imekuwa ikilielekeza kundi hili kwenda kufanya shughuli mbalimbali za kiuchumi ikiwemo kilimo pamoja na uvuvi.

Mheshimiwa Spika, kundi hili limekuwa likikabiliwa sana na changamoto ya mabadiliko ya tabianchi ambazo zimekuwa zikiathiri shughuli hizi za kiuchumi na kurudisha jitihada za vijana hawa.

Mheshimiwa Spika, swali langu, ni upi mpango wa Serikali kupanga bajeti maalum kwa ajili ya kundi la vijana ambao wanajishughulisha na shughuli za kilimo na uvuvi ambao wanapata changamoto sana za mabadiliko ya tabianchi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. LAURENT D. LUSWETULA) K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge; kwanza nimpongeze sana kwa namna anavyoendelea kuwatumikia wananchi wa jimbo lake. Ni ukweli kwamba Serikali kwanza imeendelea kuwawezesha vijana kupitia mifuko mingi ya vijana ikiwemo hata juzi mama yetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ametoa zaidi ya shilingi bilioni 200 kwenda kwenye Wizara ya Vijana. Hii yote ni kujali kwamba vijana wanafanya kazi na wanapata mitaji ya kuendesha biashara zao.

Mheshimiwa Spika, sisi kama Serikali tuseme tumejipanga vya kutosha kuhakikisha kwamba kundi hili la vijana tunaliwezesha kwa kiasi kikubwa ili lisitetereke kwa namna yoyote, waweze kujiinua kiuchumi kupitia shughuli zao wanazozifanya za kila siku.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Majule.

**MHE. DKT. NEEMA P. MAJULE:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kumuuliza swali Mheshimiwa Naibu Waziri kuwa tunatamani kushiriki kwenye huu uchumi jumuishi. Ni kwa jinsi gani Serikali imejipanga kuweza kushirikisha watu kutoka vijijini, wanawake, lakini vijana watakavyoshiriki kwenye huu uchumi shirikishi. Tukizingatia sana viashiria ambavyo vitawekwa kupima kwamba makundi haya maalumu nayo yameshiriki, hasa kupitia kutafutiwa masoko, lakini utumiaji teknolojia mpya, umilikishwaji wa ardhi, siyo hivyo tu, ikiwepo upatikanaji wa ajira zikiwepo ajira zilizo rasmi na ajira ambazo siyo rasmi, ili huu uchumi jumuishi ambao utatokea, usitokee kutoka kwa wawekezaji wakubwa, lakini na sisi watu wa chini ikiwepo wanawake tuwe tumeshirikishwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. LAURENT D. LUSWETULA) K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA**

**UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, nimshukuru sana Dkt. Neema Majule kwa swali lake la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwanza swali hili ni lazima kidogo turejee katika Dira ya Maendeleo ya miaka 25 ambayo imepita ambayo kwa kiasi kikubwa kwanza imefanya vizuri sana. Ambapo mpaka kufikia mwaka 2024, wastani wa pato la mtu mmoja mmoja limeweza kukua zaidi ya mara tatu, kutoka dola za Kimarekani 453 mpaka dola za Kimarekani 1,227 lakini pia umri wa kuishi nao umeongezeka kutoka wastani wa miaka 51 mpaka miaka 68.

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo sasa dira hii ya miaka 25 mingine inayokuja, tumejipanga kuhakikisha kwamba makundi yote ya wanawake, vijana, wafanyabiashara, wawekezaji nao wanaenda kuguswa na dira hii ya miaka 25 ambayo tunaenda kuanza nayo tarehe 01 Julai, 2026 mpaka mwaka 2050.

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo nimhakikishie kabisa Mheshimiwa Mbunge, sisi kama Serikali tumejipanga vya kutosha kuhakikisha kwamba makundi hayo ambayo ameyataja, tunaenda kuyagusa kwa kiasi kikubwa na kuyawezesha kwa kiasi kikubwa kuhakikisha kwamba wanatekeleza shughuli zao za kila siku, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hokororo.

**MHE. AGNES E. HOKORORO:** Mheshimiwa Spika, ahsante, kwa kuwa Bunge lako hili ndilo Bunge ambalo litaanza kutekeleza Mpango wa Dira ya Taifa 2050 kwa bajeti hii.

Je, Serikali imejipangaje kuhakikisha inaweka Kitengo cha Ufuatiliaji na Tathmini kwa kuwa malengo ya dira hii ni makubwa kuliko dira tuliyomaliza kuitekeleza? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. LAURENT D. LUSWETULA) K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:**

Mheshimiwa Spika, ahsante sana, nimshukuru sana Mheshimiwa Hokororo kwa swali lake nzuri la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwanza nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kama Serikali imejipanga vya kutosha na ndiyo maana imekuja na mpango wa *e-Delivery*, kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi, ambao ni mfumo wa kitaifa wa usimamizi wa mipango na miradi ya maendeleo, hii ni kama *database* ambayo sasa yenyewe itakuwa inafuatilia. Kwanza miradi yote ya maendeleo ambayo iko katika dira hii, ndio imehifadhiwa hapo, ambayo sasa itakuwa inafuatilia utekelezaji; mradi upi umekamilika, mradi upi umefikia asilimia ngapi, mradi upi unahitaji kitu gani. Ufuatiliaji kwa maana ya *planning, monitoring and evaluation*, mfumo huu ndio unaenda kumaliza kabisa changamoto hizo.

Mheshimiwa Spika, Wabunge hapa kipindi cha nyuma tulikuwa tunalalamika kidogo kwamba kuna mipango mingine na miradi mingine ambayo inaingizwa kwenye utekelezaji bila mpangilio maalumu. Sasa suluhisho ni mfumo huu wa *e-Delivery*, ambao unaenda kuhakikisha kwamba miradi yote iliyoidhinishwa ndio inakuwepo hapa. Hiyo mipango yote ikishawekwa italuwa-*locked* na hakuna mtu ambaye anaweza kuifungua. Lengo na madhumuni tusipate mradi mpya ambao haujaidhinishwa kuweza kuingiwa kwenye mpango kazi wa miradi ambayo tayari imekwisha idhinishwa.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea Wizara ya Uchukuzi, Mheshimiwa Mgore Miraji Kigera.

Na. 513

**Mwekezaji wa *New Musoma Hotel***

**MHE. MGORE M. KIGERA** aliuliza: -

Je, Serikali imefikia wapi kuhusu mwekezaji aliyeonesha nia ya kuwekeza Hoteli ya *New Musoma* ambayo ni alama ya Mji na Mkoa wa Mara?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Uchukuzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mgore Miraji Kigera, Mbunge wa Musoma Mjini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Shirika la Reli linaendelea kuboresha nyumba na majengo ya biashara pamoja na hoteli zinazomilikiwa na shirika ikiwemo Hoteli ya Musoma. Aidha, *TRC* imejidhatiti katika kuhakikisha kwamba inashirikisha sekta binafsi katika kufanya uwekezaji wa hoteli hii ili kuleta tija na kuongeza mapato ya shirika.

Mheshimiwa Spika, *TRC* ilipokea mwekezaji ambaye ameonesha nia ya kuwekeza katika Hoteli ya Musoma. Aidha, shirika limemtaka mwekezaji kuwasilisha andiko la mradi, pamoja na michoro ya maboresho anayotaraji kuyafanya. Pindi atakapokamilisha uwasilishaji wa nyaraka hizo hatua za kuendelea na majadiliano zitaanza.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mgore.

**MHE. MGORE M. KIGERA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru, kwanza napenda kutoa pongezi na shukrani za dhati kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa majibu mazuri ya kuonesha dhamira ya dhati ya kuweza kufufua ya *New Musoma Hotel*. Nina maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeonesha nia ya kuanzisha *Tourism Corridor between Serengeti National Park* na *Lake Victoria*. Je, haioni sasa umuhimu wa kuharakisha mchakato huu ili kuweza kupata mwekezaji huyo kwa uharaka. Kwa mujibu wa Naibu Waziri wa Mipango na

Uwekezaji aliwaahidi wananchi wa Jimbo la Musoma Mjini kufikia Julai, mwekezaji huyu atakuwa amekabidhiwa hoteli hiyo. Ni lini sasa Serikali itaona umuhimu wa kulifanya hili kwa uharaka?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kupitia hoteli ya *New Musoma*, itaweza kuleta watalii pamoja na wawekezaji kwa uharaka. Tuna uwanja wetu wa ndege wa Musoma, mpaka sasa haujaweza kuanza kufanya kazi. Je, Serikali inatuambia nini Wananchi wa Musoma na Mkoa wa Mara, uwanja huo lini utaanza kufanya kazi rasmi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza Mheshimiwa Mgore Kigera, kwa jinsi ambavyo anafuatilia maendeleo ya wananchi wa Musoma, wilaya au mkoa ambao ni muhimu kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, kwanza, tunatambua umuhimu huo ndiyo maana tumeshaanza mchakato Serikalini kuifufua hoteli hiyo, kushirikisha sekta binafsi, kwa sababu tunatambua kwamba pale Musoma kuna ziwa, kuna shughuli za uvuvi na usafirishaji majini, pale Musoma kuna hifadhi kwa maana ya kwamba watalii wanahitaji kupata hoteli nzuri ambayo ni ya kisasa, pale Musoma kuna madini, lakini pale Musoma kwenye Mkoa huo ndipo anapotoka baba wa taifa. Kwa hiyo, watu wengi sana wangependa kwenda katika mkoa huo.

Mheshimiwa Spika, tayari tumeshaanza mchakato huo na mhusika mmojawapo mwekezaji binafsi ambaye ameonesha nia ameshapatikana. Tutakwenda kwa ushauri wake alioutoa, ambao ndio wa Kibunge, kuongeza kasi ya majadiliano ili tufike hatima nzuri, hatimaye hoteli hii muhimu iweze kuanza kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, swali la pili; ameuliza kwamba hoteli hii itategemea pia iweze kupokea wateja au watu wanaokuja kwenye shughuli mbalimbali ambao kimsingi tunakusudia moja ya

usafiri utakaotumika ni uwanja wa ndege, anataka kufahamu ni lini utakamilika.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali hii ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, imeonesha kutambua na kuthamini umuhimu wa kuboresha Uwanja wa Ndege wa Musoma ndio maana imeidhinisha shilingi bilioni 36 na ujenzi uko 67%.

Mheshimiwa Spika, wiki iliyopita Waziri wa Uchukuzi, Mheshimiwa Profesa Mbarawa, alinituma hapa nitoe *route* mpya ya ndege zetu na miongoni mwa maeneo ambayo aliyatolea maelekezo ni pamoja na Uwanja wa Ndege wa Musoma pamoja na Shinyanga ambapo mwezi huu tunakusudia kuanza majaribio ya ndege kwenye viwanja viwili, Musoma pamoja na Shinyanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimsihi Mheshimiwa Mbunge na Wabunge wengine kuendelea kumuunga mkono Mheshimiwa Dkt. Samia, kwa sababu anazidi kuleta tabasamu kwa wananchi wake. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuweza kunipatia fursa na mimi kuuliza swali.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Tanzania tunatarajia kunufaika na uwepo wa *AFCON* na ukuaji wa utalii, na kwa kuwa wageni ambao watakuja kipindi cha *AFCON* watahitaji hoteli zenye hadhi ya nyota nne mpaka tano wengine.

Serikali ina mkakati gani wa haraka wa kuweza kufufua au kutafuta wawekezaji kwenye hoteli za umma ambazo zimetelekezwa kwa muda mrefu kama vile *Motel Agip* na *Embassy* ili ziweze kuongeza malazi, ajira na mapato ya taifa kuliko kuendelea kuwa *liability* kwa Taifa? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Esther Matiko, aliyeuliza kwa ujumla hoteli mbalimbali za Serikali.

Mheshimiwa Spika, mimi kimsingi, kwa niaba ya Waziri wa Uchukuzi, nitajikita kwenye miradi iliyopo kwenye sekta yetu. Kama ambavyo nimeshaanza kumjibu Mheshimiwa Mgore, tunatambua maeneo mbalimbali, kwanza, kwa ajili ya kuongeza ajira, ukifufua hoteli unaongeza ajira kwa wananchi, lakini pili, unaimarisha utalii. Kwa maeneo ambayo ni ya kimkakati ambapo *AFCON* inakwenda kutumika maana yake pia inasaidia kuongeza *accommodation*, wananchi waweze kupata mahali au washiriki kwenye kombe hilo, waweze kushiriki.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba ametuongezea msukumo mkubwa zaidi ya kutushauri na kutukumbusha Serikalini ili tuendelee kuona umuhimu wa kuweza kufufua maeneo hayo kwa maslahi ya Watanzania wote.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, ahsante, pamoja na *Southern Sun* siyo mali ya Serikali, lakini ni hoteli muhimu sana Dar es Salaam na imefungwa toka mwaka 2021. Kitu gani kinafanyika na kitu gani Serikali ichukue hatua ya kukwamua shida hii ya *Southern Sun*. Huna haja kulijibu, ila wewe nenda nalo. *(Makofi)*

Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Paul Mnzava.

Na. 514

**Ujenzi wa Bwawa la Mayuyu na Skimu za Umwagiliaji – Korogwe**

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itajenga Bwawa la Mayuyu na Skimu ya Umwagiliaji - Korogwe Vijijini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WA UCHUKUZI K.n.y. WAZIRI WA KILIMO** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo naomba kujibu swali la Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava, Mbunge wa Korogwe Vijijini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na utekelezaji wa miradi mbalimbali ya umwagiliaji nchini ikiwemo katika Wilaya ya Korogwe ambapo kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zinaendelea katika Skimu za Kwamngumi, Magoma, Mapangoni na Kwagunda ambapo usanifu huo unajumuisha Mabwawa ya Magoma na Mapangoni (Mayuyu) yaliyopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe. Usanifu wa mabwawa hayo umefikia wastani wa 40% kwa usanifu wa Bwawa la Magoma na 73.6% kwa usanifu wa Bwawa Mapangoni na unatarajiwa kukamilika ifikapo Novemba, 2026. Baada ya usanifu wa mabwawa hayo kukamilika utajumuishwa kwenye mpango wa ujenzi wa miradi ya umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, vilevile, Serikali inaendelea na ujenzi wa skimu za umwagiliaji katika Skimu za Mkomazi na Chekelei zilizopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe ikihusisha ujenzi wa Mabwawa ya Mkomazi na Chekelei ambapo utekelezaji wake umefikia 96.4% kwa Bwawa la Mkomazi na 10% kwa Bwawa la Chekelei. Ujenzi wa Bwawa la Mkomazi unatarajiwa kukamilika Septemba, 2026 na ujenzi wa Bwawa la Chekelei unatarajiwa kukamilika mwezi Februari, 2027.

Mheshimiwa Spika, kukamilika kwa miradi hiyo kutanufaisha wakulima 20,000 katika Vijiji vya Manga Mtindiro, Goha, Kwenangu, Magila, Mkumbara, Mazinde Mheza, Mazinde Bagamoyo, Mabogo, Kasiga, Mlembule, Magila Gereza, Mombo, Makuyuni, Kwasunga, Chekelei, Chepete, Madumu na Madala.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mnzava.

Waheshimiwa Wabunge, tupunguze foleni ya maswali ya nyongeza.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, pamoja na majibu ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza; kumekuwa na utaratibu mara nyingi wa kufanya usanifu kwa ajili ya mabwawa, lakini baada ya kukamilika usanifu wa mabwawa ndiyo kazi ya ujenzi wa skimu inafuata na jambo hili huwa linachelewesha kazi hizi. Je, Serikali haioni sasa iko haja ya usanifu wa skimu za umwagiliaji na mabwawa haya uende kwa pamoja?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; pamoja na kazi nzuri ambayo Serikali inafanya, lakini iko ahadi ya muda mrefu ambayo ilitolewa na Serikali kupitia kwa Waziri Mkuu ya ujenzi wa bwawa kwa ajili ya Skimu ya Mombo pamoja na ujenzi wa eneo la Skimu ya Kwamkumbo. Ni lini ahadi hii ya Serikali itatekelezwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI K.n.y. WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, napenda kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Timotheo Mnzava, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, la kwanza, napenda kumpongeza Mheshimiwa Mnzava ni mfuatiliaji mzuri sana wa miradi ya umwagiliaji kwenye jimbo lake, lakini na kwa nchi nzima. Kwa kweli amethibitisha jinsi ambavyo vijana wakiaminiwa wana uwezo wa kufuatilia mambo makubwa kwenye majimbo na kwenye nchi hii, ili Taifa letu liweze kusonga.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na ushauri wake ambao amesema kwamba kwa nini isiende pamoja mambo yote mawili, kwanza nipende kupokea, lakini pili, kupitia Waziri wa Kilimo, nimwombe Mkurugenzi wa Tume ya Umwagiliaji wapokee ushauri huu, uchakatwe na kama utaonekana pengine unaweza kuwa na tija, tuanze kuufanyia kazi kwa sababu lengo letu wote ni kujenga.

Mheshimiwa Spika, la pili, kuhusiana na kufufua Mto Soni, moja nipende kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali imekwisha kamilisha usanifu wa miundombinu ya umwagiliaji kwa maana ya Skimu za Mombo pamoja na bwawa. Kwa kuwa tumeshakamilisha, hatua inayofuata ni kuanza manunuzi kwa ajili ya kumpata mkandarasi huyo.

Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge baada ya kumpata mkandarasi huyu, tutakwenda kuanza utekelezaji ili wananchi wake wa Korogwe ambao kimsingi anawapenda sana, waweze kunufaika na miradi hii. Naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Mhata.

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, katika Jimbo la Nanyumbu, Kata ya Masuguru, kuna Skimu ya Umwagiliaji katika Bwawa la pale Lukula na Kijiji cha Masuguru. Upembuzi yakinifu umefanyika na umekamilika na usanifu wa kina umekwisha. Ni lini sasa ujenzi wa skimu hii utaanza ili wananchi wa kata ile waweze kunufaika na mradi huu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI K.n.y. WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mhata, Mbunge wa Nanyumbu kwa swali lake la nyongeza alilouliza kuhusiana na skimu ya wananchi wake.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali hii imetambua umuhimu mkubwa sana kwa maana ya kuboresha skimu za umwagiliaji nchini na ndiyo maana, siyo tu imeongeza bajeti ya kilimo kutoka shilingi bilioni 294 mpaka shilingi trilioni 1.1, lakini pia imeongeza bajeti nzima ya miradi yote inayotekelezwa nchini kama ambavyo kimsingi Mheshimiwa Waziri alizungumza ambapo miradi zaidi ya 886 nchi nzima ipo kwenye hatua mbalimbali, ikiwemo na ile miradi 146 ambayo naamini na ya kwake ni mmojawapo.

Mheshimiwa Spika, nimwombe Mheshimiwa Mbunge awe na subira. Iko miradi ambayo inatekelezwa na kukamilishwa, ipo mingine ambayo tunategemea kwenda kuanza, na ipo mingine tunakwenda kusaini, wakandarasi wanakwenda kusaini, lakini na mingine tunakwenda kuanza hatua za usanifu. Awe na subira, Serikali itakwenda kufikia miradi yote ikiwepo na wa kwake kulingana na upatikanaji wa fedha za Serikali.

**SPIKA:** Mheshimiwa Asia, ajiandae Mheshimiwa Ng'umbi.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Skimu ya maji ya umwagiliaji ya Kata ya Endagaw, ina zaidi ya miaka 15. Imetumia fedha za Serikali shilingi bilioni 1.5 na mara ya mwisho mkandarasi ana miaka miwili toka aondoke.

Je, ni lini Serikali itaenda kukamilisha Skimu ya Miradi ya Maji ya Endagaw, na je, Mheshimiwa Waziri uko tayari twende tukakague fedha hizi nyingi za Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ambazo ametuletea lakini bado hazijaleta matokeo chanya kwa wananchi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI K.n.y. WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Asia Halamga ambaye anawapigania wananchi wake kuhakikisha kwamba skimu ya umwagiliaji ambayo Serikali imeshaianza inakamilika.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, tunayo miradi takribani 71 ambayo ipo kwenye hatua mbalimbali, kuanzia asilimia moja mpaka 99% kuelekea 100%. Naamini mradi huu ni mmojawapo. Hapa nyuma nchi hii imekuwa na mambo mengi ya kufanya na wewe ni shahidi. Tumekuwa na fedha nyingi tumepeleka kwenye *SGR* ambayo leo Watanzania wananufaika, tumepeleka kwenye Bwawa la Mwalimu Nyerere. Nina uhakika,

baada ya kukamilisha miradi hii mikubwa, kasi ya maendeleo kwenye miradi mbalimbali ikiwemo ya maji, ukiwemo huu wa kwako itakwenda kukamilika. Naomba uwe na subira.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na ombi la kuambatana na mimi Mheshimiwa Mbunge kama Mheshimiwa Waziri wa Kilimo asipokuwa na nafasi, yeye au Naibu wake, akanituma mimi nimwakilishi, sitaweza kukataa maelekezo ya Serikali. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Ng'umbi.

**MHE. JASMINE C. NG'UMBI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, swali langu ni kuwa; je, ni nini mpango wa Serikali kuhakikisha skimu za umwagiliaji zinafika katika Mkoa wa Iringa, hususani katika majimbo yote saba, ili kuweza kuwasaidia vijana wa Mkoa wa Iringa kujiajiri, lakini pia kulima kilimo cha kisasa? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI K.n.y. WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mbunge wa Vijana, Mheshimiwa Jasmine Ng'umbi kwa jinsi ambavyo anawapigania vijana wa nchi hii. Yeye na Wabunge wenzake ambao wanawakilisha vijana hapa Bungeni wamethibitisha umuhimu wa kuwa na vijana makini wanaofuatilia masuala ya maendeleo ya vijana, kwa maslahi ya Taifa leo na kesho.

Mheshimiwa Spika, kwa swali lake ambalo kimsingi anauliza kwa upande wa Mkoa wa Iringa kwamba ni lini skimu hizi zitakamilika.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa katika mkoa wetu wa Iringa, Wizara ya Kilimo inatekeleza miradi mbalimbali ikiwa ni pamoja na uchimbaji wa visima virefu karibu kwenye majimbo yote saba katika mkoa wetu. Pili, tuna miradi takribani 24 ambayo ipo kwenye hatua mbalimbali ya usanifu, lakini tatu, tunayo miradi mbalimbali, ikiwa ni pamoja na Mradi wa Ruaha Mbuyuni, Mradi wa Mgololo, Mradi wa Mkombozi na Miradi mingine, ambayo kimsingi inatekelezwa. Serikali inampa uhakika Mheshimiwa

Mbunge na Wabunge wote ambao wanataka kufahamu kuhusiana na Mkoa wa Iringa na maeneo mengine, itakwenda kuongeza kasi kuhakikisha kwamba maeneo hayo, au wananchi wa Mkoa wa Iringa hususani vijana ambao yeye anawawakilisha, wanakwenda kunufaika ili washiriki kwenye uzalishaji, wapate ajira, wajenge uchumi na waweze kusaidia shughuli mbalimbali katika familia zao.

**SPIKA:** Mheshimiwa Emmanuel.

**MHE. EMMANUEL J. KHAMBAY:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, je, ni lini Serikali itakamilisha zoezi la upembuzi yakinifu juu ya ujenzi wa bwawa la umwagiliaji katika Kata ya Bagara, hususani eneo la Kijiji cha Nakwa ili wananchi wa eneo hilo waweze kunufaika na kilimo cha umwagiliaji?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI K.n.y. WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, napenda kujibu swali la nyongeza kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge ameweza kuuliza kwamba kama nilivyosema hapo awali, nimtoe mashaka Mheshimiwa Mbunge. Kasi ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ni kuhakikisha kwamba, wananchi wake wananufaika na nchi hii na ameamua kukifanya kilimo kuwa uti wa mgongo.

Mheshimiwa Spika, ili kukamilisha hoja hiyo, eneo la umwagiliaji, ambalo wakati anaingia yeye madarakani lilikuwa ni eneo dogo sana la kumwagilia, takribani eneo la hekta laki sita, wakati Mungu ametupa fursa ya eneo lenye ukubwa zaidi ya hekta milioni 40. Ninakuhakikishia Mheshimiwa Mbunge na ukawaambie na wananchi, Waziri wa Kilimo anawaambia, atakwenda kuwafikia maeneo yote ambayo ni ya kimkakati ili wananchi waweze kuzalisha na tuweze kuuza nje ya nchi na ndani ya nchi chakula pamoja na mazao mbalimbali.

**SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Fedha, Mheshimiwa Kafiti.

Na. 515

**Kukamilisha Kanuni za Bima za Kilimo**

**MHE. KAFITI W. KAFITI** aliuliza: -

Je, lini Serikali itakamilisha Kanuni za Bima za Kilimo ili kuongeza na kupatikana kwa kinga kwa wakulima na mazao mbalimbali?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. LAURENT D. LUSWETULA)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, ahsante sana na kwa niaba ya Waziri wa Fedha, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kafiti William Kafiti, Mbunge wa Jimbo la Ilemela, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na utafiti kuhusu bima katika mnyororo wa kilimo yaani mazao, mifugo, misitu na uvuvi ili kwa pamoja na mambo mengine kuwa na kanuni zinazovutia uwekezaji katika bima ya kilimo na kuweka mazingira wezeshi kwa wakulima ili kupata huduma za bima kwa urahisi na haraka. Ni mpango wa Serikali kukamilisha uandaaji wa kanuni hizi katika kipindi cha mwaka 2026/2027. Naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Kafiti.

**MHE. KAFITI W. KAFITI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali na sasa naomba niulize swali la nyongeza.

Kwa kuwa kilimo ndiyo uti wa mgongo wa uchumi wa nchi yetu na umeajiri wananchi wengi katika nchi yetu ya Tanzania, kwa hiyo suala la kinga ya bima kwao ni ulinzi mkubwa juu ya

kilimo wanachokifanya, na kwa kuwa suala hili limeshachukua muda mrefu, sasa nini kauli ya Serikali juu ya ukamilishwaji wa kanuni hizi ili ziweze kusaidia wananchi wetu? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. LAURENT D. LUSWETULA):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza nikiri, ni kweli kabisa kilimo ndicho kimeajiri Watanzania wengi sana ambao wanajipatia kipato na kulingana na umuhimu wake na ndiyo maana kiukweli tumechukua muda mrefu ili kujiridhisha kwamba hizi kanuni zitakuwa rafiki kwa wakulima na Watanzania wote ambao wanajihusisha na kilimo. Kwa maana hiyo, kama ambavyo nimeweza kujibu kwenye jibu langu la msingi, mwaka huu wa fedha utakaonza 2026/2027 ndipo tunaenda kukamilisha utafiti huu na kanuni hizo zitaanza kutumika. Naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Nollo.

**MHE. KENNETH E. NOLLO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, pamoja na nia njema ya Serikali ya kutaka kuleta bima katika sekta ya kilimo na mifugo, lakini nataka niulize, kwenye suala zima la mifugo; ni masuala gani makubwa ambayo, kwanza yanaleta tatizo kubwa la kutopata bima ili kabla ya kufikiria kutengeneza kanuni mmeyaona mrekebishe ili kwamba hata mtu akitaka kupata bima isiwe na *risk* kubwa zaidi katika suala hilo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. LAURENT D. LUSWETULA):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, kwanza, kuja na kanuni hizi maana yake hata sisi wenyewe kama Wizara, kuja na hii bima ya kilimo tumeona kabisa kwamba kuna umuhimu wake. Ndiyo maana kabla ya kuingia, kwa maana ya kuleta kanuni, tukasema tufanye utafiti kwa kushirikiana na wadau ili tuweze kupata maoni yao nabaada sasa ya kupata maoni yao, tukishakamilisha, ili tuje

sasa na bima ambayo, sasa itakuwa na utekelezaji ambao ni imara.

Mheshimiwa Spika, kwa namna hiyo, nipende tu kumhakikishia Mbunge ya kwamba hapo awali hatukuwa na bima hizo, lakini baada ya kuona sasa kuna umuhimu wa kuwa na bima hizo za kilimo ikiwemo ufugaji na ndiyo maana tukasema kwa haraka na kuchukua jukumu la haraka kufanya utafiti na kwa sababu tuko mwishoni, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge ya kwamba baada tu ya kumaliza, tutafanya mipango mingine na kwa kukaribisha maoni mengine ya wadau, ili kama pengine kanuni zile zina mapungufu, basi tuweze kuzirekebisha kulingana na maoni mengine mapya ya wadau.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ngajilo.

**MHE. FADHILI F. NGAJILO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, nilitaka kuuliza kwamba, kwenye hizi kanuni ambazo zitaundwa kwa ajili ya bima ya mifugo na kilimo; je, wakulima wadogo au wafugaji wadogo wameshashirikishwa kwa namna gani, kwa sababu tuna tatizo kwenye ufugaji, wafugaji wetu wanapoteza sana mifugo yao kutokana na magonjwa na ajali ambazo zinatokea. Je, sasa wanaingizwa vipi katika mfumo huo wa kupata hizo bima ili tuokoe mitaji hii ya wafugaji wadogo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. LAURENT D. LUSWETULA):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza nimhakikishie Mbunge kwamba wakulima hawa wadogo ambao anawazungumzia na wao pia ni miongoni mwa wadau ambao tayari tumekwishawashirikisha kuhusu bima hii ya kilimo. Wao wametoa maoni yao na kwa kipindi chote ambacho sisi kama Wizara ya

Fedha tumekuwa tukitembea kwenye halmashauri mbalimbali kutoa elimu ya kifedha, moja ya ajenda pia ambayo tunaibeba ni hii bima ya kilimo.

Kwa hiyo, nimhakikishie kwamba, hata maoni ya wadau na wakulima wadogo haya, nayo yamezingatiwa na kanuni hizi ambazo sasa zitaanza kutumika katika mwaka huu wa fedha 2026/2027. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Lucy Mwakyembe.

**MHE. LUCY EDWARD MWAKYEMBE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi kuuliza swali la nyongeza na nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri ya Serikali kwa ajili ya uanzishwaji wa bima hii ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kilimo ndiyo suluhisho la kumkomboa Mtanzania katika ajira, wakiwemo vijana, je, Serikali inaonaje kuongeza kasi ya utafiti katika kukamilisha na kutumika bima hiyo hasa kwa upande wa bima ya mazao, mvua nyingi, ukame, wadudu kwenye mimea, pamoja na dhoruba. Matukio haya yanasababisha wananchi kupata majanga ya asili ambapo bima ikianza kwa haraka walau itampunguzia maumivu mwananchi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. LAURENT D. LUSWETULA):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza, nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa swali zuri la nyongeza, kwanza bima hii ya kilimo, nikiri kabisa kwamba imeanza kama miaka miwili au miaka mitatu huko nyuma. Kwa maana hiyo, katika hali ya kawaida kulingana na maoni ya wadau ambayo tumeendelea kuyapokea mpaka sasa hivi, jambo hili na utafiti huu ulitakiwa uchukue muda mrefu zaidi wa miaka hii miwili au mitatu ambayo sisi kama Wizara ya Fedha tunaweza kutumia.

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo, yeye ameuliza kwamba kuona namna ya kuweza kuharakisha; kwanza sisi kama

Wizara ya Fedha tumeharakisha na kwa sababu hiyo, kama nilivyojibu kwenye swali langu la msingi, uharakishwaji huo na ndiyo maana tunaenda kutekeleza zaidi, kanuni hizi katika mwaka wa fedha 2026/2027 kuanzia Julai 1, 2026.

**SPIKA:** Ahsante. Wizara ya Ujenzi. Mheshimiwa Moses Charles Bujaga.

Na. 516

**Ujenzi wa Barabara ya Malya – Nyambiti (Kilometa 58)**

**MHE. MOSES C. BUJAGA** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga kwa kiwango cha lami Barabara ya Malya – Nyambiti (kilometa 58) ili kuboresha usafirishaji katika Jimbo la Sumve?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI K.n.y. WAZIRI WA UJENZI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Moses Charles Bujaga, Mbunge wa Sumve, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wakala ya Barabara Tanzania *(TANROADS)* inaendelea na kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya Malya – Nyambiti, kilometa 58 kwa ajili ya kuijenga kwa kiwango cha lami. Baada ya usanifu kukamilika na gharama za ujenzi kufahamika, Serikali itatafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami.

**SPIKA:** Mheshimiwa Moses Charles.

**MHE. MOSES C. BUJAGA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, barabara hii ya Fulo - Nyambiti – Malya ilitakiwa kukamilika huo upembuzi yakinifu na

usanifu wa kina kufikia mwezi wa Aprili, 2026. Ningependa kufahamu ni kwa nini kazi hiyo haijakamilika mpaka sasa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili, barabara hii kwa sasa iko katika hali mbaya sana na ndiyo inayobeba uchumi wa Jimbo la Sumve, minada ya Bungulwa, usafirishaji wa mazao kama dengu na pamba ambayo ndiyo msimu wa sasa hivi utakuwa ni changamoto. Serikali ina mpango gani kuhakikisha barabara hii inapitika, ili kurahisisha usafirishaji wa mazao na usafiri wa wananchi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI K.n.y. WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, napenda kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Moses Charles Bujaga, Mbunge wa Sumve, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, awali napenda kumpongeza kwa jinsi ambavyo amekuwa ni mtu wa shukrani ya kutambua kazi nzuri ambayo inafanywa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwenye eneo lake, lakini pili, amekuwa ni mfuatiliaji makini, kwa huu muda mfupi wote tunashuhudia, anavyopigania barabara za jimbo lake na hata za mkoa wake kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, ameuliza kwa nini haijakamilika katika muda uliokuwa umepangwa; moja, mhandisi mshauri alikuwa ameshakamilisha ile kazi, lakini kama unavyofahamu, mahitaji yanazidi kuongezeka. Timu ya wataalam ikapitia na kubaini kwamba kuna mambo mengine ambayo yakiongezwa, yatakuwa na maslahi mapana zaidi kuliko walivyofikiria pale awali na kimsingi jambo hili ni jambo jema kwa sababu pengine barabara ya awali ilikuwa inakusudiwa, ilitazamiwa kwa mahitaji ya pale mwanzoni.

Kwa hiyo, wataalamu wakaona iko haja kufanya maboresho, ili barabara itakayofikiwa kuamuliwa kujengwa, iendane na ndoto na matamanio ya yeye Mbunge, wananchi na Taifa letu kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, nimwombe awe na subira, kwa sababu baada ya hatua hii sasa, tumemwongezea mkandarasi muda, angalau mpaka kabla ya mwezi wa Agosti au kabla ya mwaka huu haujaisha ili kazi hii iwe imekamilika.

Mheshimiwa Spika, la pili; ameuliza kwamba barabara hii imekuwa ni mbovu ambayo kimsingi sisi Serikali tunakubaliana na yeye na tunampa pole kwa changamoto hiyo, kawaida barabara hii itakiwa ifanyiwe ukarabati mara mbili kwa maana mwezi wa 10 pamoja na mwezi Mei mpaka Juni. Mwaka jana mwezi wa 10 ukarabati mzuri ulifanyika, sasa kipindi kama hiki ambacho wakulima na wananchi wanakusudiwa kusafirisha mazao mbalimbali kama vile pamba, dengu na mazao mengine barabara hiyo kweli ni mbovu.

Mheshimiwa Spika, tayari taratibu zimeshaanza kufanyika ili mkandarasi huyu sasa aingie kazini hivi karibuni na namwelekeza kwa Niaba ya Waziri wa Ujenzi amenituma nimwelekeze Meneja wa *TANROADS* ili alisimamie jambo hili mkandarasi huyo aingie kazini, aanze kufanya kazi na aboreshe barabara hii ili wananchi wa Sumbe na Mkoa wa Mwanza na maeneo jirani kwa ujumla waweze kunufaika na barabara hii na kujenga uchumi wao.

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Suma, ajiandae Mheshimiwa Simon.

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Rungwe kuna barabara ya muhimu sana inayotoka Kiwila, Kinyala inapita Isangati inatokea Mbalizi. Barabara hiyo wananchi wanateseka sana namna ya kusafirisha mazao yao na kusafiri wao wenyewe hasa wanawake.

Mheshimiwa Spika, je, ni lini barabara hiyo itajengwa kwa kiwango cha lami?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI K.n.y. WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Suma Fyandomo, Mbunge kutoka Mkoani Mbeya anayewakilisha kina mama kwa jinsi anavyowapigania Wananchi wa Mkoa wa Mbeya wakiwemo wa Rungwe, wakiwemo wa Kyela, Mbozi, Chunya na maeneo mengine yote na kimsingi barabara hii sisi kama Serikali tunatambua umuhimu wake.

Mheshimiwa Spika, nimwombe Mheshimiwa Suma Fyandomo pamoja na Wabunge wa majimbo wa maeneo hayo na wananchi kwa ujumla wawe na subira, Serikali inatambua umuhimu wa barabara hii na maeneo mengine ni muhimu yakajengwa kiwango cha lami, lakini kwa sasa sungura ni mdogo tujipe muda wakati utafika itajengwa na watafurahia.

**SPIKA:** Mheshimiwa Simon Songe Lusengekile.

**MHE. SIMON S. LUSENGEKILE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Tunayo barabara ya kutoka pale Nyashimo kwenda Dutwa Wilaya ya Bariadi kupitia pale Maliri, Shigala, Ngasamo pamoja na Dutwa yenyewe inayounganisha wilaya mbili na tumekuwa tukiahidiwa kujengwa kwa kiwango cha lami.

Je, ni lini Serikali sasa itaanza ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami kwa ajili ya uchumi wa hizi wilaya mbili?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI K.n.y. WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi swali la Mheshimiwa Songe ambaye anaielezea barabara hiyo yake muhimu na nipende kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge pamoja na Wabunge wengine wote kwa sababu naamini eneo hili ni eneo nyeti sana Serikali inatambua umuhimu wa barabara katika uchumi wa Taifa lake na kwa sasa kama ambavyo Waziri wa Ujenzi amesimama mara kadhaa tupo kwenye mchakato Serikalini, kwanza ya kutambua wakandarasi ambao walikwishaanza kazi wamesimama, wakandarasi ambao walikwishaanza kazi

walisimama na ambao pengine mikataba yao hawajisainiwa lakini pia maeneo mengine ambayo bado hayajasainiwa na yanayotakiwa kutangazwa.

Mheshimiwa Spika, niwahakikishieni mlimsikia mwenyewe Mheshimiwa Waziri Mkuu akizungumza hapa na naomba tuwe na subira Waheshimiwa Wabunge. Barabara hizi baada ya kuwa tumeshafanya kazi nzuri ya kusimamia uchaguzi wenyewe kwa hela zetu kujenga Daraja la Busisi, kujenga *SGR,* kujenga Bwawa la Mwalimu Nyerere na kufanya mambo mengine mengi makubwa ninayo hakika Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan anakwenda kujenga barabara mbalimbali kwenye nchi hii zikiwemo hata zile za kule Mufindi ambazo tunazipigania kila wakati.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zacharia

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Barabara ya Mlima Magara katika Jimbo la Mbulu Mjini barabara yenye jiografia ngumu sana, na kwa kuwa mkandarasi aliyekuwa anajenga zege katika Mlima Magara amesimama kwa muda wa zaidi ya mwaka moja; ni lini mkandarasi atarudi *site* ili akamilishe zege katika Mlima Magara?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI K.n.y. WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kufuatilia barabara yake muhimu ambayo kimsingi mkandarasi alikuwa *site* kama alivyoeleza amesimama.

Mheshimiwa Spika, mara tutakapokamilisha taratibu za fedha tukishamlipa mkandarasi huyo atarejea kufanya kazi na wewe Mheshimiwa Mbunge na wananchi tunaomba muwe na subira kwa kipindi hiki.

**SPIKA:** Mheshimiwa Josephine Chagula.

**MHE. JOSEPHINE T. CHAGULA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona, barabara inayotoka Kahama kupitia Nyang'hwale mpaka Busisi ni barabara muhimu sana kwa biashara na uchumi wa Mkoa wa Geita. Je, ni lini Serikali itajenga barabara hii kwa kiwango cha lami?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI K.n.y. WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, Serikali inayo dhamira ya kuhakikisha wananchi wanaopita kwenye barabara hiyo inayotokea Kahama wanaboreshewa barabara hiyo, lakini kwa sasa kwa kuwa fedha hazipo tunaomba wananchi wavumilie, tunaendelea na mchakato Serikalini pale itakapokuwa tayari Serikali itakwenda kujenga kwa kiwango cha lami.

**SPIKA:** Mheshimiwa Midimu, ajiandae Mheshimiwa Mama Salma.

**MHE. ESTHER L. MIDIMU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, barabara ya kutoka Bariadi kwenda Lamadi ina hali mbaya sana, ina mashimo na mabonde imebomoka bomoka. Je, ni lini Serikali itafanya ukarabati wa barabara hiyo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI K.n.y. WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi namwelekeza Meneja wa *TANROADS* wa Mkoa huo wa Simiyu aende atazame barabara ambayo imelalamikiwa na Mheshimiwa Mbunge ili atazame kiwango cha uharibifu na kisha kuweza kuweka mpango wa namna bora ya kuweza kuikarabati ili Serikali na wananchi waendelee kunufaika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Salma Kikwete.

**MHE. SALMA R. KIKWETE:** Mheshimiwa Spika, je, ni lini Barabara yetu ya Milola - Kiwawa, Milola - Kutwa itajengwa kwa kiwango, mimi sihitaji lami mimi nahitaji changarawe na hizi barabara ni muhimu sana na hizi barabara umuhimu wake mkubwa ni sehemu ambayo inazalisha ufuta kwa kiwango kikubwa sana na ukubwa wa barabara hii ni kilometa sita tu. Je, lini Serikali itatupatia pesa kujenga barabara hizi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI K.n.y. WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi ninamwelekeza Meneja wa *TANROADS* aende akaone eneo hilo la kilometa sita ambalo limelalamikiwa au limeombewa na Mheshimiwa Mbunge kwamba lina usumbufu na hivyo linahatarisha biashara ya ufuta pamoja na wananchi kupita kwenye maeneo hayo na kwa msingi Mbunge anatimiza jukumu la msingi la Kibunge la kuishauri na kuisimamia Serikali na sisi Serikali hii ya Mheshimiwa Dkt. Samia wakati wote tumesisitizwa kuwa wasikivu kwa sauti za Wabunge na mara baada ya kujua mahitaji halisi basi Serikali itachakata na kuwa namna bora kuweza kufanyia kazi ombi la Mheshimiwa Salma Kikwete, Mbunge kama alivyoomba.

**SPIKA:** Tuaendelea Mheshimiwa Salum Khamis Salum.

Na. 517

**Utekelezaji wa Mradi wa Barabara ya Nkoma – Makao Kilometa 65**

**MHE. SALUM K. SALUM** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itaanza utekelezaji wa Mradi wa Barabara ya Nkoma – Lalago kilometa 65?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI K.n.y. WAZIRI WA UJENZI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi napenda kujibu swali la Mheshimiwa Salum Khamis Salum, Mbunge wa Meatu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mkataba wa ujenzi kwa kiwango cha lami wa Barabara ya Nkoma – Lalago kilometa 65 umesainiwa kati ya Serikali na Kampuni ya ujenzi ya *China Civil Engineering Construction Corporation (CCECC)*. Serikali inaendelea na taratibu za malipo ya awali ili kuwezesha mkandarasi kuanza kazi za ujenzi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Salum.

**MHE. SALUM K. SALUM:** Mheshimiwa Spika, ahsante, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini tu kumkumbusha kwamba barabara hiyo imewekwa kwenye ilani safari ya tatu hii ilani tatu na siku zote inakosa fedha. Sasa ni muhimu mkajua umuhimu wa barabara hiyo kusudi bajeti hii itengewe fedha na mkandarasi aanze.

Mheshimiwa Spika, pili, barabara hiyo inakutukutanisha sisi Mkoa wa Simiyu pamoja na Mkoa wa Singida kwa Daraja kubwa la Mto Sibiti, Daraja la Sibiti lilivyojengwa lilikuwa lina kilometa 24 za lami ambazo *contractor CHICO* alishapewa mkataba huo, kwa hiyo, tunaiomba tena Wizara impe fedha mkandarasi *CHICO* kusudi ajenge kilometa 24 ambazo kilometa zingine zitakuwa kwa Mkoa wa Singida na zingine Mkoa wa Simiyu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI K.n.y. WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi nampongeza Mheshimiwa Salum Khamis Salum kwa kuendelea kufuatilia miradi ya kimkakati ikiwemo barabara hii muhimu sana kwa uchumi na maisha ya wananchi wake.

Mheshimiwa Spika, kimsingi kama alivyosema barabara hii imekuwa ikiahidiwa mara kadhaa kwenye Ilani ya CCM, lakini pamoja na kuahidiwa mara kadhaa kwenye ilani za huko nyuma

ni wajibu wetu yeye mwenyewe Mheshimiwa Mbunge na Wabunge wote kuweza kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuamua sasa kwanza kuijenga, kitendo cha kusaini mkataba na kampuni ya *CCECC* ni dhamira ya dhati kwamba Serikali sasa imeamua inaenda kuijenga.

Mheshimiwa Spika, na kwa sasa kama ambavyo tumesema kwenye majibu ya msingi Serikali baada ya kuwa imeshasini mkataba inafanya taratibu za kutafuta fedha Serikalini.

Mheshimiwa Spika, nimwombe Mheshimiwa Mbunge pamoja na wananchi kwa ujumla wawe na subira dhamira ya Serikali ya kuijenga barabara hii kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge mara kwa mara anakumbushia iko pale pale, subira yavuta kheri, tutaifikia barabara hiyo kuijenga vizuri na wao watafurahia.

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Kangi Lugola.

**MHE. KANGI A. LUGOLA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Barabara ya kutoka Busambara hadi Mugara - Iramba zaidi ya miaka 10 tuliomba iingizwe kwenye huduma ya *TANROADS* na tunaambiwa mchakato unaendelea zaidi ya miaka 10.

Sasa je, ni lini mchakato huu utakamilika kwa sababu barabara hii inaendelea kuharibika sana na mpaka sasa magari hayapiti? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI K.n.y. WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Kangi Lugola kwa kukumbushia ombi lake muhimu, ninaomba awe na Subira, wakati Serikali inaendelea na mchakato wa kina wa kuona namna bora ya kuweza kuihudumia barabara hiyo, na mara baada taratibu zitakapokamilika Serikalini basi ombi la Mheshimiwa Kangi Lugola litakwenda kukamilika.

**SPIKA:** Mheshimiwa *Engineer* Ramadhani, ajiandae Mheshimiwa Lukuba.

**MHE. RAMADHANI H. SINGANO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Barabara ya Mombo – Soni - Lushoto ni barabara ya kimkakati kwa majimbo matatu. Ni lini Serikali itaona umuhimu wa kuipanua barabara hii ili kukidhi haja katika eneo hili?

**SPIKA:** Mheshimiwa waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI K.n.y WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, nimpongeze Mheshimiwa Mbunge pia kwa kufuatilia barabara yake ambayo ni muhimu kwa sababu barabara ndiyo mishipa ya uchumi wa nchi yetu, lakini muombe awe na subira. Tutaendelea na mchakato Serikalini itakapokuwa tayari tutakwenda kuikamilisha na hivi ndivyo tunakwenda Serikalini kwa vipaumbele, baada ya kumaliza hatua moja tunakwenda hatua nyingine barabara moja tunakwenda barabara nyingine.

**SPIKA:** Asante. Mheshimiwa Morris.

**MHE. MORRIS J. MAKOI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Kagongwa – Igusule - Mwamara mpaka Nzega imeshajengwa mpaka tabaka la tatu kutoka Kagongwa kwenda Igusule kilometa 18.3 kilichobaki ni kuwekwa lami kipande hicho cha kilometa 18.3. tukikiacha kitaharibika.

Mheshimiwa Spika, sasa Serikali ina mpango gani wa kukamilisha uwekaji wa lami kilometa 18.3 kutoka Igusule kwenda Kagongwa ili kuokoa thamani ya fedha iliyotumika hadi sasa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI K.n.y WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Morris kwa

kukumbushia barabara yake muhimu kama ambavyo nimesema kwenye majibu ya msingi, Serikali inayo dhamira ya dhati na inawahakikishia Wabunge wote ikiwemo Mheshimiwa Mbunge huyu miradi yote ambayo tumekwisha kuianza tutakwenda kuikamilisha na ile ambayo tunakusudia kuianza Serikali inakwenda kuikamilisha.

Mheshimiwa Spika, naomba awe na subira kwa kuwa tumeshaonesha nia, Serikali imekwisha anza ujenzi hata kipande hicho Serikali itakwenda kukikukamilisha ili kuwaweza kusikiliza kilio na maombi ya wananchi wa eneo hilo kama ambavyo imewasilishwa na Mheshimiwa Mbunge leo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Cherehani.

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, barabara inayotoka Mkunze inaenda Iponyang'olo - Ilamba, Igwamanoni inapakana na wenzetu wa Masumbwe ni barabara ambayo imepanda kwenda *TANROADS* leo miaka minne, lakini haijawahi kutengewa fedha na wala hawajafika hata kuikagua. Ni nini mkakati wa Serikali juu ya barabara hiyo?

**SPIKA:** Mheshimiwa waziri,

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI K.n.y WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa uvumilivu wake pamoja na kwamba anasema barabara yake haikutengewa fedha na kwa kweli anafuatilia sana maendeleo ya jimbo lake, wilaya yake na sekta zote.

Mheshimiwa Spika, nimwombe Mheshimiwa Cherehani vuta subira. Serikali hii imefanya mambo mengi na makubwa zaidi haitashindwa kujenga barabara za nchi hii ikiwemo ya kwako. Tujipe muda hatua kwa hatua, tutaifikia barabara yake na yeye atafurahi pamoja na wananchi kama ambavyo tumekwisha fanya kwenye maeneo mengine ya maji, umeme pamoja na sekta zingine ndani ya jimbo lako.

**SPIKA:** Mheshimiwa Shayo.

**MHE. IBRAHIM M. SHAYO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Mheshimiwa Naibu Waziri umekuwa ukiniambia kila siku tarehe 01 Juni, mkandarasi ataingia *site* kuhusu barabara ya Mailisita kuelekea Kiboroloni ya njia nne. Je, ni lini unawaambia wananchi wa Moshi Mjini mkandarasi ataingia *site*?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI K.n.y WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Shayo kwa jinsi ambavyo anakumbushia barabara hii. Endelea kuvuta subira Mheshimiwa Shayo, tunakamilisha taratibu za kifedha ndani ya Serikali kama ambavyo Serikali hii imefanya mengi kwenye Jimbo la Moshi na wewe unafahamu kwenye uwanja wa ndege tumepeleka mabilioni pale, nataka nikuhakikishie hata hii vuta subira tutakwenda kufika na wananchi wa Moshi watafurahia.

**SPIKA:** Mheshimiwa maswali yetu yamekwisha, sasa kipindi hiki cha wageni.

Wageni Waheshimiwa Wabunge, wapo wageni tisa wa Mheshimiwa Zainab Rashid Kawawa, Wajumbe wa Baraza la UVCCM wastaafu mwaka 2008 hadi 2012, karibuni. *(Makofi)*

Wageni 47 Mheshimiwa Johannes Lembulung' Lukumay kutoka Kituo cha Kulelea Watoto Yatima cha *The Joy of God Open Centre* cha Jijini Arusha, karibuni. *(Makofi)*

Wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; wapo wanafunzi 102 na walimu watatu wa Shule ya Sekondari ya Don Bosco ya Mkoani Iringa, karibuni. *(Makofi)*

Katibu wa Bunge anapenda kuwatangazia Waheshimiwa Wabunge kwamba kufuatia uhitaji wa viwanja vya Waheshimiwa Wabunge naomba kuwajulisha kuwa Jiji la Dodoma lina viwanja katika eneo la Nala na Kikombo. Hivyo kwa wale wanahitaji viwanja wanaomba kufika Kliniki ya Ardhi iliyopo katika viwanja

vya Bunge ili waweze kusaidiwa kufungua akaunti mfumo wa *TAUSI* zitakazowezesha kupata viwanja hivyo.

Aidha, kwa wale wanahitaji viwanja Mtumba bado mchakato unaendelea na pale utapokamilika mtatangaziwa ili kuweza kuomba viwanja hivyo kupitia mfumo wa *TAUSI*. Taarifa muhimu zinazohitajika wakati wa kufunga akaunti ni namba ya Kitambulisho cha *NIDA*.

Waheshimiwa Wabunge, tangazo lingine Kamati ya Uongozi na Kamati ya Bajeti inaendelea kukutana tena katika kujadili mambo mahususi yalijitokeze katika mijada wa bajeti na Kamati zingine zote zitaendelea na kazi kwenye Kamati zao kama zilivyopangwa.

Waheshimiwa Wabunge, ninaahirisha Shughuli za Bunge mpaka kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 5.16 Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Ijumaa, Tarehe 5 Juni, 2026 Saa Tatu Asubuhi)*